# Nipashe

Jumamosi Januari 25, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581932

www.ippmedia.com

Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


UKURASA 2

# Lissu aweka kiporo hatima ya kina Mdee



UKURASA WA 3

**Waziri** akiri migogoro ya ndoa bado ni pasua kichwa



UKURASA WA 4

**Neema** yawaangukia makandarasi wazawa, walipwa mabilioni wanayoidai serikali



UKURASA WA 5

**JK** aonya wanaotumia dini kujenga chuki, faraka



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza wakati wa hafla ya utoaji wa Tuzo za Mlipakodi Bora wa Mwaka 2023/24, Dar es Salaam juzi. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 24

## SIMBA SASA HESABU KUBEBA TAJI LA CAF

NAHODHA wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', amefichua malengo ya timu na wachezaji wa timu hiyo waliojiwekea msimu huu ni kufika hatua ya fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika ...



## Ugonjwa Marburg waua mtu mmoja

UKURASA 2

# Samia akemea rushwa ulipaji kodi

• **Ateua,** atengua Ma-DC, Ma-DED... *Endelea Ukurasa 3 & 4*

MICHEZO YANGA: COPCO FC MTATUSAMEHE UK.24 MAONI, UK.6

# Abiria 300,000 wasafiri kwa SGR ndani ya siku 44

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

ZAIDI ya abiria 300,000 wamesafiri kwa treni ya Reli ya Kisasa (SGR) ndani ya siku 44, hivyo kufanya hadi sasa idadi ya waliopanda tangu ianze huduma kati ya Dar es Salaam na Dodoma Agosti, 2024 kufikia watu milioni 1.5.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika stesheni ya Dodoma ambao walikuwa wakijiandaa kusafiri kwenda katika mkutano wa msemaji huyo utakaofanyika leo Hifadhi ya Taifa ya Mikumi, Morogoro.

Msigwa alisema takwimu hizo zinaonesha ni wastani wa abiria 300,000 kwa mwezi wanasafiri na kusisitiza kuwa, zipo treni za kutosha kutoa huduma ya usafiri kwa wananchi.

Alisema vichwa vya treni 17 na mabehewa zaidi ya 78 yameingia na serikali imejipanga kutoa huduma ya vizuri kwa wananchi.

"Matatizo yanayojitokeza kwenye usafiri huu ni ya kawaida lakini pia, kuna hujuma za miundombinu tumeendelea kuchukua hatua na kuhusu umeme tatizo linalojitokeza mara moja, linatokana na shida Gridi kwenye yote ya Taifa," alisema.

Alisema serikali inaendelea na ujenzi wa vipande vingine kwa awamu na lengo ni kukamilisha mradi huo ili kutoa huduma na utakapokamilika utakuwa umegharimu Sh. trilioni 23.

Hata hivyo, alisema serikali inakamilisha maandalizi ya kuanza kusafirisha mizigo kwa kipande mikoa ya Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam.

Msigwa alisema treni moja itakuwa na uwezo wa kubeba tani 10,000 na tayari mabehewa 264 yamewasili na mengine 264 yapo bandarini wakati wote yatashushwa.



Aliyekuwa Balozi, Dk. Wilbroad Slaa akiwa chini ya ulinzi wa maofisa wa magereza alipofikishwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana kwa ajili ya kusikiliza maombi ya uhalali wa yeye kunyimwa dhamana katika shtaka linalomkabili la kuchapisha taarifa za uongo katika mitandao ya kijamii. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Lissu aweka kiporo hatima kina Mdee

**Na Restuta James**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameweka msimamo kuhusu wabunge 19 wa Viti Maalum, akiwamo Halima Mdee, kwamba hatima yao inategemea mkutano mkuu wa chama hicho.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Lissu alisema ili wabunge hao ambao walifutiwa uanachama mwaka 2022 warejee CHADEMA, inabidi kuitisha kikao cha mkutano mkuu.

Hata hivyo, kwa mujibu wa Ibara ya 7.7.9 ya Katiba ya CHADEMA, Mkutano Mkuu unafanyika kila baada ya miaka mitano. Kwa mantiki hiyo, Mkutano Mkuu wa chama hicho utafanyika mwaka 2030 kwa kuwa ulimalizika Januari 22, 2025 wakati wa uchaguzi wa viongozi wakuu na waandamizi wa chama hicho.

Alisema kama wabunge hao wana dhamira ya kurudi kwenye chama hicho, wanapaswa kujiandaa kujieleza namna walivyoingia bungeni bila idhini ya Katibu Mkuu wa chama.

"Hawajawahi kusema hizo fomu za kugombea nani aliyewapa na kuzisaini wakati zinapaswa kusainiwa na Katibu Mkuu pekee, na John Mnyika hakuwahi kuzitia saini," alisema.

Alisema baadhi ya wabunge hao walitokea gerezani na kuibukia bungeni, na kwamba chama kitahitaji kujua aliyewapelekea fomu gerezani.

"Kwa hiyo kama wanakuja kutaka suluhu na chama, waje wafungue siri za mioyo yao. Waje na mioyo myeupe na tuichunguze ni myeupe kweli. Wasije tu kwa sababu uchaguzi umekaribia kutaka ubunge," alisema.

Mbali na Mdee, wabunge waliofukuzwa ni Ester Bulaya, Esther Matiko, Cecilia Pareso, Jesca Kishoa, Sophia Mwakagenda, Grace Tendega, Conchesta Rwamlaza, Nusrat Hanje na Taunza Malapo.

Kamati Kuu ya CHADEMA iliwafukuza Mdee na wenzake kwa utovu wa nidhamu kwa kosa la kuapishwa kuwa wabunge bila ruhusa ya chama chao.

Baadaye Mkutano Mkuu wa chama hicho ulibariki uamuzi huo jambo lililowafanya wakimbilie mahakamani kulinda ubunge wao.

Hata hivyo, baada ya mvutano mahakamani, CHADEMA kilishinda lakini hadi sasa wabunge hao bado wako bungeni.

Kuhusu ukomo wa viti maalum ya udiwani na ubunge kwa chama hicho, Lissu alisema mabadiliko ya katiba ya CHADEMA pamoja na kanuni, yataweka ukomo wa miaka mitano na baada ya hapo watapaswa kugombea kwenye majimbo.

Katika hatua nyingine, ushindi wa Lissu siku ya Jumanne umevuta hisia za mashabiki wa chama hicho, huku mawakili 11 wakijiunga CHADEMA.

Katibu Mkuu wa chama hicho, John Mnyika, aliiambia Nipashe jana kwamba kumekuwa na mwamko mkubwa wa wananchi wa kada mbalimbali kujiunga, huku hamasa kubwa ikifanyika mitandaoni.

"Tumeona mwamko mkubwa sana kwenye mitandao ya kijamii watu kutaka kujiunga na chama, siwezi kusema wamejiunga kwa kiwango gani, ni hadi tukusanye takwimu kutoka maeneo mbalimbali," alisema.

Mmoja wa mawakili waliojiunga na CHADEMA, Matojo Kosatta, alisema wasomi hao wamejiunga kwa kuwa wanaamini chama hicho kinaweza kupigania maslahi mapana ya Watanzania. "Ni kweli tumejiunga na kuna mawakili wengine watajiunga awamu ya pili. Tunaamini Mwenyekiti wetu (Tundu Lissu), atakipeleka chama katika mwelekeo mzuri. Yale mambo ambayo tulikuwa tunataka yafanyike tunaamini yatafanyika kwa sababu tulikuwa tunatoa ushauri, lakini ukawa haufanyiwi kazi," alisema.

# Ugonjwa Marburg waua mtu mmoja

**Na Jenifer Gilla**

WIZARA ya Afya, imesema mtu mmoja amefariki dunia kwa ugonjwa wa Marburg mkoani Kagera, wakati akiendelea na matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo.

Mtu huyo alikuwa kati ya wawili waliobainika awali kuwa na ugonjwa huo na kulazwa hospitalini hapo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani humo, Mkurugenzi wa Kinga Wizara ya Afya, Dk. Ntuli Kapologwe, alisema kifo hicho kilitokea Januari 21, mwaka huu, na mmoja anaendelea na matibabu na afya yake inaendelea vizuri.

Dk. Kapologwe alisema wanaendelea kuwafuatilia kwa siku 21 watu 281 ambao walichangamana na watu waliothibitika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo ili kuona kama wataonesha dalili zozote.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Grace Magembe, alisema idadi ya wahisiwa inabadilika kulingana na watu wanaokwenda kutoa taarifa wanapohisi kuwa na dalili na hadi jana, wahisiwa walifika 15.

Dk. Magembe alisema wahisiwa hao walifanyiwa kipimo kimoja ambacho hakikuonesha kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo na watarudia baada ya saa 72.

Alisema dalili za ugonjwa huo zinafanana na za magonjwa mengine kama vile malaria, maambukizi kwa njia ya mkojo (UTI) na magonjwa ya tumbo.

Alisema kutokana na hali hiyo, watu wakienda hospitalini kwa magonjwa mengine wanawapima na ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Dk. Magembe, idadi ya wahisiwa inabadilika kila siku kutokana na idadi ya watu watakaojitokeza kupima wakijihisi kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Alisema licha ya kuthibitika kuwapo kwa ugonjwa huo katika kata mbili za wilaya ya Biharamulo, hatua zote stahiki za kujikinga na ugonjwa huo zimechukuliwa na watu wanaendelea na shughuli zao kama kawaida. "Hii inatuonesha kwamba tunaweza kuendelea na shughuli wakati tukizingatia kanuni zote za afya ambazo zinatusaidia tusieneze haya maambukizi," alisema.

Januari 20, mwaka huu, Shirika la Afya Duniani (WHO) liliipatia Tanzania Sh. bilioni 7.55 ili kudhibiti na kukabiliana na ugonjwa huo.

Januri 21, mwaka huu, akizungumza na waandishi wa habari Ikulu ya Chamwino, Dodoma, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwahakikishia Watanzania na jumuiya ya kimataifa kuwa Tanzania ni eneo salama licha ya kubainika kisa kimoja cha mtu mmoja kupata maambukizi hao. Alisema hatua zilizochukuliwa kudhibiti virusi hivyo vilipobainika nchini mwaka 2023 zimeiwezesha Tanzania kuwa na uzoefu wa kutosha kudhibiti maambukizi.

HABARI KITAIFA

# Samia akemea rushwa ulipaji kodi

Na Romana Mallya

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa maagizo kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda, kuhusu masuala ya ulipaji kodi na wanaotengeneza mazingira ya rushwa.

Amemtaka kuchukua hatua za haraka kwa watumishi wanaotengeneza mazingira ya kutokuwa na usawa katika ulipaji wa kodi na yanayochochea rushwa.

Kadhalika, ametaka mtumishi yeyote anayejihusisha na vitendo hivyo visivyofaa kwa maendeleo ya nchi kushughulikiwe.

Rais Samia alitoa maagizo hayo juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa hafla ya utoaji tuzo za shukrani kwa Mlipakodi Bora wa Mwaka 2023/24 zilizotolewa na TRA, huku akimsisitizia Kamishna Mwenda kusimamia usawa katika kulipa kodi.

Vilevile, Rais Samia alimwelekeza kiongozi huyo kuchunguza mienendo ya watumishi na kuchukua hatua za haraka na bila upendeleo kwa mtumishi yeyote anayejihusisha na vitendo vya rushwa ikiwamo kusaidia ukwepaji kodi.

"Ukwepaji kodi unaathiri wananchi, wafanyabiashara na nchi kwa ujumla, kusababisha kuchelewesha maendeleo ya nchi na kuifanya serikali kushindwa kutekeleza mipango yake ya maendeleo kwa wakati kama ilivyokusudiwa," alisema.

Rais alisema dhamira ya serikali ni kuendelea kujenga mazingira wezeshi ya watu kufanya kazi, biashara na uchumi kuendelea kukua, ili kupata kodi kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma za jamii na ustawi wa watu.

Alisema kwa kuzingatia dhamira hiyo, mwaka 2024 aliunda Tume ya Maboresho ya Kodi ili ifanye tathmini ya mfumo wa kodi na kuleta mapendekezo ya namna ya kuboresha mfumo huo.

"Lengo la tume hii ni kujenga mfumo wa kodi unaoimarisha usawa katika kulipa kodi, unaotabirika, ulio rahisi na usio na usumbufu na wenye viwango vya kodi rafiki," alisema.

Rais Samia alisema serikali imedhamiria kuwa na mfumo wa kodi unaorahisisha na kuchagiza shughuli za kiuchumi ili kodi ikusanywe kwa wingi, kuleta maendeleo kwa haraka zaidi na kupunguza utegemezi wa kibajeti.

Kuhusu matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Rais Samia aliitaka TRA kutumia mifumo hiyo katika kumhudumia kwa wakati mlipakodi wa mwisho na kuongeza mapato ya kikodi yanayoendana na uwekezaji uliofanywa katika kujenga uchumi wa kidijitali na kuwarahisishia walipakodi kutimiza wajibu wao.



Fundi Mkuu wa karakana ya watu wenye ulemavu Dodoma (KAWADO), Mwita Marwa, akitengeneza baiskeli ya magurudumu matatu kwenye kiwanda chake, kilichopo katika Soko la Sabasaba, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kuwauzia wateja wake. Baiskeli moja ikikamilika inauzwa kwa 600,000/- hadi Sh. milioni 1.3. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri akiri migogoro ya ndoa pasua kichwa

Na Augusta Njoji

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, ametaja maeneo manne yenye kadhia kubwa kwenye mikoa 11 iliyofikiwa na Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MSLAC).

Ameyataja maeneo hayo kuwa ni migogoro ya ndoa, migogoro ya ardhi, mirathi na ukatili wa kijinsia.

Akizindua jana kampeni hiyo mkoani Kigoma, itakayofikia vijiji 240 ndani ya siku tisa, Dk. Ndumbaro alisema katika mikoa 11, wananchi 775,119 wamefikiwa na kupokea na kusikiliza migogoro 3,162.

Alisema katika awamu hii kampeni hiyo itafanyika mikoa sita na hivyo kuifikia mikoa 17, huku akibainisha kuwa kwa Mkoa wa Kigoma eneo ambalo linaonekana kuwa na kadhia ni tatizo la uraia.

Kutokana na changamoto hiyo, Dk. Ndumbaro, amemwagiza Kamishna Jenerali wa Uhamiaji kuweka banda la uhamiaji ili wananchi wasikilizwe na wenye haki ya kupatiwa uraia wapewe.

Kadhalika, amemwagiza Kamishna Msaidizi wa Ardhi Mkoa wa Kigoma kuwa kila eneo ambalo kampeni itafanyika kuwe na banda la watu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ili kusikiliza kero na migogoro ya wananchi na wanaohitaji hati wapate.

Alisema moja ya changamoto iliyoko kwenye mirathi ni watu kuogopa kuandika wosia wakiamini ni kujichuria kifo wakati kuna watu wameandikia wosia na bado wapo hai.

"Wosia si kifo ni matakwa yako wewe endapo Mungu atakuchukua unataka familia yako iishi vipi wakati haupo. Hapa sisi wote tutakufa haijulikani ni lini, sasa ikitokea unataka nyumba au shamba lako liwe vipi, wosia ni jambo muhimu kama unaitakia mema familia yako na ni la wote wanawake na wanaume," alisema.

Kuhusu kamati za msaada wa kisheria wilaya na mikoa, alisema maeneo mengi hazifanyi kazi ipasavyo zimelala hivyo, kupitia kampeni hiyo, elimu inayotolewa ni kuzifufua ili msaada wa kisheria uratibiwe ngazi ya mikoa hadi mitaa.

Waziri huyo alisema zaidi ya asilimia 54 ya sheria zote zimebadilishwa lugha kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

"Rais Samia ametuletea elimu ya msaada wa kisheria na msaada wa kisheria kwa wale wenye changamoto bure kwa wote wenye uhitaji ili kupata haki zao. Uzinduzi huu niliofanya Kigoma mikoa mingine sita itakayofikiwa na kampeni awamu hii ni Katavi, Tabora, Mtwara, Geita na Kilimanjaro," alisema.

Naye Mbunge wa Kigoma Mjini, Kilumbe Ng'enda, alisema kampeni hiyo ni muhimu kwa wananchi wa Kigoma kwa kuwa wengi wao wanapoteza haki kwa kukosa msaada wa kisheria.

"Moja ya haki zinazosumbua watu ni haki za kiraia, kuna watu wanakosa baadhi ya haki za kisheria kwasababu wanashindwa kujua utaratibu wa kukana uraia wa mzazi mmoja ambaye si raia wa Tanzania kunasababisha leo akose kitambulisho cha NIDA, leseni ya udereva, biashara na kukimbizana na vyombo vya dola," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Dk. Rashid Chuachua, alisema kampeni hiyo itakuwa chachu ya maendeleo na itaweka mazingira wezeshi kwa wananchi kufanya shughuli zao bila hofu na wananchi wapo tayari kupokea msaada huo wa kisheria.

Awali, akizungumza kwa niaba ya Waziri Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, Naibu Katibu Mkuu, Amon Mpanju, alisema kampeni hiyo inakwenda kutatua migogoro mingi kwa jamii.

Kadhalika alisema inakwenda kusaidia kujua namna ya kuzifikia haki zao na inatekeleza mpango wa kukabiliana na ukatili wa wanawake na watoto.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kutoka Zanzibar, Yusfa Abdalla Said, alisema ofisi hiyo inatarajia kuzindua kampeni hiyo katika mikoa ya Unguja na Pemba Februari, mwaka huu.

Mwakilishi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Baraka Mbwilo, alisema TLS inamuunga mkono Rais Samia kwa kuanzisha kampeni hiyo ili kuwafikia wananchi kutoa msaada wa kisheria.

# Mtoto aliyeibwa apatikana yu hai

Na Jenifer Gilla

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani limewakamata watu watatu wakiwa na mtoto wa miezi saba, Merysiana Melkzedeck, wanaodaiwa kumwiba kwa wazazi wake katika tukio la uvamizi lililotokea Januari 15, mwaka huu.

Tukio hilo lililotokea saa moja asubuhi Galagaza, Kata ya Msagani, wilayani Kibaha, mkoani Pwani. Watu wanne wakiwa na mapanga na nondo walimvamia nyumbani kwake na kumjeruhi mfanyabiashara Melkizedeck Sostenes (28).

Watu hao pia, walimfunga kamba na kumtumbukiza kwenye shimo la maji taka kisha kumchukua mke wake, Johana Gabriel na mtoto huyo na kuondoka nao kusikojulikana.

Vilevile, watu hao waliiba gari dogo aina ya IST lenye namba za usajili T.331 DLZ, runinga aina ya Haier nchi 42, kompyuta mpakato tatu na simu tano za aina mbalimbali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi (ACP) Salim Morcase, alisema baada ya msako waliwakamata watuhumiwa hao jana saa 9:00 alfajiri wakiwa wamejificha katika msitu ulioko kati ya eneo la Kimara Misale na Serengeti "B" Kata ya Dutumi.

Alisema mtoto aliyepatikana alipelekwa Hospitali ya Rufani Tumbi kwa uchunguzi zaidi.

"Jeshi la Polisi tulifanikiwa kuwakamata watuhumiwa watatu ambao walihusika katika tukio hili wakiwa na mtoto wa kike mwenye umri wa miezi saba akiwa hai waliomchukua katika tukio la uvamizi la 15/01/2025," alisema.

Pia alisema Jeshi la Polisi lilifanikiwa kukamata gari lililoibwa katika uvamizi huo, pete ya ndoa ya mke wa Melchizedek, simu aina ya Redmi na kompyuta mpakato moja.

Alisema baada ya kupokea taarifa ya uvamizi huo, Kamanda Morcase aliambatana na wataalamu wa kuchunguza matukio makubwa ambapo walifika eneo la tukio na baada ya kupata taarifa msako ulifanyika na kukamatwa kwa wahalifu na kupatikana mama na mtoto waliochukuliwa.

"Mke wa Melchizedek alipatikana saa 10:00 jioni akiwa ametumbukizwa katika shimo la nyumba ya jirani umbali wa mita 300, ambalo halikuwa limeanza kutumika," alisema.

Morcase alisema upelelezi unaendelea ikiwamo kusakwa kwa mtuhumiwa mmoja, huku Jeshi la Polisi likitoa wito kwa wananchi kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu haraka kwa viongozi walioko maeneo yao ili hatua za haraka zichukuliwe.



Waziri wa Afya, Jenista Mhagama (katikati), akipiga makofi, baada ya kuzindua Kliniki ya Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), tawi la Oysterbay, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Samia ateua, atengua Ma-DC na Ma-DED

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi, uhamisho na mabadiliko ya viongozi mbalimbali huku akiteua na kutengua uteuzi wa wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Dk. Moses Kusiluka, Rais amemteua Godfrey Mnzava kuwa Mkuu wa Wilaya ya Moshi kuchukua nafasi ya James Wilbert Kaji aliyeteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Kabla ya uteuzi huo, Mnzava alikuwa Ofisa Tarafa wa Ilemela.

Michael Semindu aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Iringa ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbulu kuchukua nafasi ya Veronica Arbogast Kessy ambaye amestaafu na Khamana Simba ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ulanga kuchukua nafasi ya Dk. Julius Ningu ambaye amestaafu.

Awali, Simba alikuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Arusha.

Rais pia amemteua Hamad Rajabu Mbega, aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbozi na Peter Nicholaus Masindi, Katibu Tawala wa Wilaya ya Mkalama, kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu.

Aidha Rais pia amefanya uhamisho wa wakuu kadhaa wa wilaya. Waliohamishwa ni Joseph Mkude kutoka Kishapu kwenda Arusha kuchukua nafasi ya Felician Mtahengera ambaye uteuzi wake umetenguliwa; Joachim Nyingo kutoka Kilolo kwenda kuwa Bahi na Rebecca Msemwa kutoka Bahi kwenda Kilolo.

Wengine ni Hassan Bomboko kutoka Ubungo kwenda Hai; Lazaro Twange kutoka Hai kwenda Ubungo; Kisa Kasongwa kutoka Njombe kwenda Makete na Juma Sweda kutoka Makete kwenda Njombe.

**MAKATIBU TAWALA WILAYA**

Rais pia amemhamisha Jacob Rombo aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbogwe kwenda kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Arusha kuchukua nafasi ya Khamana Simba ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ulanga.

Pia amewateua Benard Urasa aliyekuwa Ofisa Tawala Mkuu, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Iringa kuchukua nafasi ya Semindu ambaye anakuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbulu.

Paul Faty, Mhadhiri Chuo cha Serikali za Mitaa, Hombolo ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbogwe kuchukua nafasi ya Jacob Rombo ambaye amehamishiwa Arusha kuendelea na wadhifa huo. Happyness Sulle, Mkuu wa Kitengo cha Maktaba na Nyaraka wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Mkalama kuchukua nafasi ya Masindi aliyeteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kishapu. Aidha, Glory Absalum, Ofisa Tarafa ya Bashnet, Babati ameteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama kuchukua nafasi ya Hamad Mbega ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbozi.

**UTEUZI MA-DED**

Edwin Bayona, aliyekuwa Mkuu wa Kitengo cha Sheria, Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe kuchukua nafasi ya Saada Mwaruka ambaye atapangiwa majukumu mengine.

Mwingine aliyeteuliwa ni Christina Bunini, aliyekuwa Mkuu wa Utawala na Rasilimali Watu, Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kuchukua nafasi ya Mhandisi Stephano Kaliwa ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Dk. Mwinyi Omary Mwinyi, Mtakwimu Mwandamizi, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo; na Alphaxard Etanga, Meneja wa Maendeleo ya Biashara na Wateja, Benki ya Exim, ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Naye Erica Yegela, aliyewahi kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mji wa Masasi ameteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuchukua nafasi ya Paul Sweya ambaye amestaafu; huku Pili Kitwana, aliyekuwa Mkuu wa Utawala na Rasilimaliwatu, Manispaa ya Morogoro ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara.

Katika uteuzi huo, Zahara Michuzi amehamishwa kutoka Halmashauri ya Mji wa Ifakara kwenda kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu kuchukua nafasi ya Athuman Masasi ambaye uteuzi wake umetenguliwa; na Loema Peter amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo kwenda Mvomero kuchukua nafasi ya Linno Mwageni ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Beatrice Clever Mwinuka amehamishwa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwenda Kilosa kuchukua nafasi ya Michael Gwimile ambaye uteuzi wake umetenguliwa; huku Siwema Juma akihamishwa kutoka Chemba kwenda Kilolo na Hassan Mnyika akitoka Kilolo kwenda Chemba;

William Makufwe amehamishwa kutoka Makete Kaliua; Jerry Mwaga kutoka Kaliua kwenda Makete; Kastori Msigala kutoka Manispaa ya Iringa kwenda Ikungi; na Justice Kijazi kutoka Ikungi kwenda Manispaa ya Iringa.

Katika hatua nyingine, Rais Samia amemteua Yokbeth Myumbilwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kuchukua nafasi ya Prof. Justinian Ikingura ambaye amemaliza muda wake.

# Neema makandarasi, walipwa mabilioni wanayoidai serikali

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAZIRI wa Ujenzi, Abdallah Ulega, amesema serikali imeanza kupunguza deni la makandarasi la zaidi ya Sh. bilioni 300 kwa kulipa zaidi ya Sh. bilioni 145, huku kipaumbele kikiwa kwa wazawa.

Ulega alisema hayo jana jijini hapa wakati akikagua ujenzi wa vivuko vipya vitano kati ya sita vinavyoundwa na mkandarasi mzawa wa Kampuni ya Songoro Marine.

"Jambo la kipaumbele kwa Rais Samia Suluhu Hassan alilonipa mimi pamoja na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ni kuhakikisha hatulali usingizi mpaka tulipe madeni ya makandarasi hasa wa ndani.

"Wakati mimi ninakabidhiwa wizara hii Desemba, deni lilikuwa Sh. bilioni 300. Ndani ya mwezi mmoja, Rais Samia ameshusha deni hilo mpaka Sh. bilioni 200 na habari njema jana (juzi) amelipa Sh. bilioni 45 na sehemu ya fedha hizo zipo za makandarasi wa ndani," alisema Ulega.

Alisema wanaamini ndani ya miezi miwili, deni hilo la ambalo limekuwa sugu kwa muda mrefu na likisemwa na makandarasi wa ndani, litakuwa limemalizwa.

"Matokeo yake ni kwamba barabara zilikuwa zimesinzia zitaanza kwenda mbio katika ujenzi wake, vilevile na uchumi wa Watanzania utazidi kuinuka kutokana na fedha hizo zinazolipwa kuongeza mzunguko wa fedha ndani," alisema Ulega.

Kuhusu vivuko, Ulega alisema serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa vivuko vipya sita pamoja na ukarabati wa vivuko vitatu ndani ya Ziwa Victoria, Bahari ya Hindi, Ziwa Tanganyika na Nyasa kwa zaidi ya Sh. bilioni 56. Pia alisema kati ya vivuko hivyo, vivuko vipya vitano vinavyotekelezwa katika Ziwa Victoria vinagharimu zaidi ya Sh. bilioni 50 na kati ya hivyo, vinne vinatarajiwa kukamilika kabla ya Machi, mwaka huu.

Alisema kivuko kimoja kinajengwa Dar es Salaam huku vinavyofanyiwa marekebisho ni pamoja na MV. Magogoni, MV. Kigamboni na MV. Nyerere.

"Nimpongeze mkandarasi huyu mzawa kwa kuendelea kufanya kazi nzuri na kuaminiwa na serikali kutekeleza miradi mikubwa na kufanikisha kwa uaminifu mkubwa," alisema Ulega.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Songoro Marine Transport Ltd, Meja Bakari Songoro, alisema utekelezaji wa vivuko hivyo utakamilika hivi karibuni.

"Kivuko cha Bwiro-Bukondo chenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 100 kimefikia asilimia 91.3 kitakamilika Machi, 31 mwaka huu. Nyegezi-Busorya asilimia 84.5 kinakamilika Marchi 29, Nyakariro-Kome 83.19 kinakamilika Machi, 29, Buyagu-Mbarika 88 kinakamilika Julai 4," alisema Songoro.

Alisema hadi vivuko vitano vya Ziwa Victoria kukamilika watakuwa wanaidai serikali Sh. bilioni 12.417.

Mbunge wa Sengerema, Khamis Tabasamu, alisema uhitaji wa vivuko katika eneo lake bado ni mkubwa.

Alisema kutekelezwa kwa kivuko cha Buyagu-Mbarika chenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 100 za mizigo kitasaidia kupunguza vifo vya wananchi zaidi ya 30 wanaofariki dunia kila mwaka kutokana na tatizo la usafiri majini.

## Dk. Malasusa aahidi serikali ushirikiano shughuli za maendeleo

**Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa, amesema kanisa hilo lipo tayari kushirikiana na serikali katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kimaendeleo nchini.

Dk. Malasusa ambaye ni Askofu wa KKKT Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP) aliyasema hayo juzi wilayani hapa wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa Mradi wa USAID Kizazi Hodari Kanda ya Kaskazini Mashariki unaosimamiwa na KKKT.

Alisema kanisa hilo liko tayari kufanya kazi na serikali na kuomba ushirikishwaji kwenye maeneo ambayo yanahitajika katika kufanya kazi za utume, hasa kundi la watoto, vijana, wanawake na wenye uhitaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, Binuru Shekidele, alisema kupitia mradi huo unaotekelezwa katika Kata ya Igulumuki, utasaidia walengwa kuinuka kiuchumi.

Katibu wa Kikundi cha Umoja Igulumuki, Yunis Zacharia, alisema kilianzishwa mwaka 2022 kikiwa na wanachama 23 wanawake na kimefanikiwa kuwafungulia watoto watatu bima ya afya kwa ajili ya matibabu.

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri hiyo, Nyajinge Julius, alisema Mradi wa USAID Kizazi Hodari Kanda ya Kaskazini Mashariki ulipokewa wilayani humo Oktoba, 2023 na umewafikia walengwa 4,992.

Lengo la kuanzishwa kwake ni kuboresha huduma za afya, ustawi na ulinzi na usalama kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wenye umri wa kuanzia miaka 0-17 na wanawake wanaonyonyesha wanaoishi na VVU.

# JK aonya wanaotumia dini kujenga chuki

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk.Jakaya Kikwete amewaonya Watanzania kuacha kutumia mwamvuli wa dini kujenga chuki na kuleta mifarakano katika jamii hali inayochochea machafuko na uvunjifu wa amani.

Kikwete ambaye ni mwasisi wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania (JMAT), alisema hayo mjini Morogoro wakati wa kikao cha kamati ambapo akawaasa viongozi wa dini kusimama imara kuhakikisha Tanzania inaendelea kubaki kuwa kisiwa cha amani, utulivu na umoja.

Alisema amani na utulivu kamwe haviwezi kununuliwa dukani badala yake ni lazima Watanzania waendelee kuimarisha undugu na mshikamano na kuepuka kubaguana kwa misingi yoyote ikiwamo ya kiimani, rangi wala kabila.

Alitolea mfano chachu ya kushauri uanzishaji wa taasisi hiyo enzi za serikali aliyoiongoza kuwa kulisababishwa na mgogoro wa kidini ulioibuka wa kuchinja, kati ya waumini wa kiislam na kikristo ambapo licha ya kuanzia eneo dogo la Katoro, watu waliusambaza na kuuchochea kuwa wa kiimani na kuleta machafuko, mauaji, majeruhi na uharibifu wa mali.

"Hali ilikuwa mbaya, kila mmoja akachukua upande wake, ikabidi tuanze kuwadhibiti watu na hata vyombo vya habari vilivyoonekana kuchochea mgogoro na ndio kama alivyosema Sheikh Alhad (Sheikh Alhad Mussa Salum, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania) tukaitisha mkutano mkubwa sana kuwahi kutokea kwa kuwashirisha viongozi wa dini zote, wakala na kulala pamoja ili kila mmoja amzoee mwenzake na ikawa mwanzo wa kuanzisha chombo hiki," alisema Rais huyo Mstaafu.

> **"Hali ilikuwa mbaya, kila mmoja akachukua upande wake, ikabidi tuanze kuwadhibiti watu na hata vyombo vya habari vilivyoonekana kuchochea mgogoro na ndio kama alivyosema Sheikh Alhad**

Mstaafu Kikwete akaielekeza taasisi hiyo kuendelea kusimamia, amani, maadili na utulivu na kusaidia utatuzi wa changamoto ya migogoro ya wakulima na wafugaji na kukiri tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo mwaka 2015 migogoro hiyo imepungua.

Aidha, akataka waongeze nguvu ili vijana wa Tanzania waishi katika mila na desturi za Tanzania na kuondokana na changamoto ya uvunjifu wa amani, kwani bado kuna changamoto kwenye malezi hivyo wasimamie ili vijana wasiharibike na utandawazi.

Akakemea baadhi ya vyombo vya habari vinavyotumika kuchochea uvunjifu wa amani na kwamba havitavumilia hali hiyo.

Mwenyekiti wa JMAT, Sheikh Alhad Mussa Salum alisema taasisi hiyo haina lengo la kufanya ibada za dini mseto na sio chombo cha dini kama baadhi ya watu wanavyofikiria.

Alisema kinachofanyika ni kuwaunganisha viongozi wa dini pamoja na kutafuta amani na utulivu wa nchi huku kila dini ikiendelea kuabudu kwa imani yake na kila mmoja anafahamu imani yake na kuiishi.

Sheikh Alhad pia akawahimiza viongozi wa dini kufanya matendo mema kwani wao wanafananishwa na chumvi ambayo ni kiungo muhimu ambayo ikichafuka haiwezi kusafishwa na kitu chochote.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima alisema mkoa wa Morogoro miaka ya zamani ulikuwa ukisifika kwa migogoro ya ardhi na wakulima na wafugaji ambapo tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo sifa hiyo haipo tena.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini JMAT, Azim Dewji alisema jukumu la kulinda amani ni la kila mmoja na hata vyama vya siasa ni yeme vikalinda hili na kufanya siasa ya staha kwasababu Tanzania ni yetu sote.




Kazi ya kuondoa taka zilizokwama ili maji ya mvua yapite kwa urahisi, ikiendelea katika Mto Mbezi, eneo la daraja la Makongo, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mwarobaini wakaidi huduma za fedha waja

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WATOA huduma za fedha nchini wametakiwa kufuata sheria na taratibu za Benki Kuu ya Tanzania (BoT), ikiwamo kujisajili, kutoza viwango sahihi vya riba na kuwapa nakala za mikataba wakopaji baada ya wao kuelewa mkataba wa makubaliano ya kukopa na kutia saini.

Kwa kufanya hivyo wataepuka adhabu mbalimbali zitakazotolewa kwa wanaokiuka sheria za huduma za fedha.

Onyo hilo limetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha, Selemani Msumi, ofisini kwake alipokutana na kufanya mazungumzo na timu ya wataalamu wa kutoa elimu ya fedha kutoka Wizara ya Fedha na taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali.

Alisema serikali inaendelea kufanya uchunguzi kuwabaini wanaofanya biashara ya kutoa huduma za fedha bila leseni, huku akisisitiza kuwa watakaobainika kukiuka sheria na taratibu za huduma ndogo za fedha hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

"Mtu yeyote anayeendesha biashara ya kukopesha pasipo kufuata taratibu, pasipokuwa na leseni hilo ni kosa na ni wizi kama wizi mwingine. Tumeshaanza oparesheni ya kuhakikisha wanaokopesha bila kuwa na leseni na ambao hawafuati sheria na taratibu tunawakamata," alisema. Akitoa elimu ya fedha kwa wajasiriamali na wananchi wa Kata ya Ilikiding'a katika Shule ya Sekondari Ilikiding'a, wilayani Arusha, Ofisa Usimamizi wa Fedha, Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Salim Kimaro, aliwataka wajasiriamali kusajili vikundi vyao vya huduma ndogo za fedha ili kulinda fedha zao dhidi ya wanakikundi wasio waaminifu.

"Hatusemi vile vikundi vyenu ambavyo havijasajiliwa mvivunje hapana. Ni vizuri ila nendeni mkavisajili kama wale mliowaona kwenye filamu wangesajili kikundi chao na kuweka benki fedha zao zisingepotea," alisema Kimaro.

Lulu Mesikana, ambaye ni mmoja wa wajasiriamali waliohudhuria mafunzo hayo ya elimu ya fedha, aliipongeza Wizara ya Fedha kwa kuona umuhimu wa kutoa elimu hiyo kwa wananchi huku akiomba programu hiyo ya elimu ya fedha iwe endelevu.

"Tunashukuru sana kwa semina hii na tukitoka hapa sasa tutakuwa makini na tutalinda fedha zetu ili tusipate hasara kama walivyoibiwa fedha wale tuliowaona kwenye filamu ya elimu ya fedha," alisema Mesikana.

Naye Ofisa Mwandamizi, Uchambuzi Fedha, Idara ya Sera, Utafiti na Mipango, kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), CPA. Gladness Mollel, aliwashauri wajasiriamali hao kuwekeza katika njia mbalimbali zikiwamo zile walizofundishwa na wataalamu wa elimu ya fedha kwa ajili ya kujikimu katika kila hali ya maisha.

"Kuna njia nyingi za uwekezaji ikiwamo hatifungani. Kuna aina mbalimbali za hatifungani, kwanza ziko hatifungani za serikali na pia hatifungani za kampuni na taasisi zingine," alisema Mollel.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi CHAN yaendelee kwa miundombinu na kikosi

**FAINALI** za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), sasa zitafanyika kuanzia Agosti, mwaka huu huku wenyeji wakiwa ni Tanzania, Kenya na Uganda.

Nchi hizo tatu za Afrika Mashariki zilitangazwa kuwa mwenyeji wa fainali hizo baada ya kushinda maombi waliyowasilisha ambayo yalibeba jina la 'Pamoja Bid'.

Awali fainali hizo zinazoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zilitarajiwa kuchezwa kuanzia Februari Mosi hadi 28, mwaka huu.

Huku kukiwa na taarifa za maandalizi kufikia zaidi ya asilimia 90, lakini huu muda ambao umepatikana kufuatia michuano hiyo kusogezwa mbele utumike vyema kwa kuboresha kila kitu ambacho CAF ilielekeza.

Inafahamika CAF hutoa maelekezo maalumu kwa kila idara inayotarajiwa kuhusika ili kufanikisha fainali hizo kufanyika katika kiwango cha juu, hivyo tutumie 'mwanya' huu uliopatikana kukamilika mahitaji yote.

Kukamilisha maandalizi kwa upande wa miundombinu, isiwe tu katika maeneo ambayo yatatumiwa na timu, maofisa na wageni watakaokuwa nchini wakati huo wa mashindano, lakini tutumie pia kujifunza kufikia ubora wa kimataifa kwa kila huduma itakayotumika katika fainali hizo.

Wakati awali ukaguzi wa mwisho wa miundombinu ambayo ni pamoja na viwanja vya kuchezea mechi na vile vya mazoezi ulitarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu, sasa ukaguzi huo utafanyika Machi, huu ni wakati wa kuendelea kumaliza 'viporo' vya ukarabati unaohitajika.

Wataalamu na mafundi wanaofanya kazi katika maeneo hayo husika, hawatakiwi kupunguza kazi, wanatakiwa kuendelea kukamilisha majukumu waliyopewa na muda wa ukaguzi utakapofika, kila kitu kiwe kwenye ubora na viwango vya kimataifa kama mwongozo unavyoelekeza.

Wakati miundombinu ikiendelea kufanyiwa kazi, huu ni wakati mwingine kwa Idara ya Ufundi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) na benchi la ufundi la Timu ya Taifa (Taifa Stars), kuhakikisha mapendekezo yake ya maandalizi yanafanyika kwa kiwango kile kile ilivyopendekeza.

Kutekeleza mambo yote ya msingi yaliyopendekezwa na Idara ya Ufundi pamoja na Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Morocco, kutakifanya kikosi kuwa imara kuelekea fainali hizo, kikosi chake kuimarika na kujiweka tayari na michuano kikiwa kamili.

Kuwa na kikosi imara, ndio njia pekee ya kutarajia kupata matokeo chanya, tutahitaji kuimarisha na kukiboresha kikosi cha Taifa Stars kwa vitendo ili kufikia ndoto za kuvuka hatua ya makundi kwa mara ya kwanza au kulibakisha Kombe la CHAN hapa Tanzania.

Wakati Serikali na TFF wakiendelea na mchakato wa kukamilisha mahitaji muhimu, pia huu ni wakati muhimu kwa mashabiki kujiandaa kwa ajili ya kujitokeza kwa wingi kuishangilia Taifa Stars katika mechi zake zote na kuonyesha uzalendo wa timu hiyo.

Kama ambavyo mashabiki hujitokeza kuziangalia timu zao wanapocheza kwenye viwanja vya nyumbani au husafiri kuzifuata klabu kuzishangilia zinapokuwa ugenini, huu ni mwaka wa kuweka rekodi kwa sababu fainali hizi za CHAN zinafanyika kwa mara ya kwanza hapa Tanzania.

Inafahamika na unatambulika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ni moja ya viwanja ambavyo mashabiki hujaa, kama inavyezekana wakati wa mechi za dabi, Tamasha la Simba Day na Siku ya Mwananchi, huu ni wakati mwingine wa kuwafanya wachezaji wa Stars wajisikie wanadeni la kupambana kusaka matokeo chanya.

Inawezekana kila mmoja kutekeleza majukumu yake na kuzifanya fainali za CHAN mwaka huu kuwa bora kutokana na wenyeji kuyabeba vyema mashindano hayo.

Tunamaliza kwa kuitakia maandalizi mazuri Taifa Stars.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Wachezaji wapewe uraia kwa maslahi ya Stars, si vinginevyo

**MOJA** ya sakata lililogonga vichwa vya mashabiki wa wadau wa soka nchini kuanzia katikati ya wiki ni uamuzi wa kupewa uraia wa Tanzania kwa wachezaji wa Singida Black Stars inayoshiriki Ligi Kuu Bara.

Wachezaji hao ambao sasa wanatambulika ni raia wa Tanzania ni Emmanuel Kwame Keyekeh, Josephat Arthur Bada na Mohamed Damaro.

Ilianza juzi kama utani au vibonzo katika mitandao ya kijamii kama ilivyo kawaida, lakini baadaye klabu hiyo ilithibitisha ni kweli wachezaji wao Keyekeh aliyekuwa raia wa Ghana, Bada (Ivory Coast) na Damaro, aliyetokea Guinea, waliomba wenyewe uraia katika mamlaka husika.

Baadaye ikatoka taarifa kutoka kwa Msemaji Mkuu wa Idara ya Uhamiaji, Paul Mselle, akithibitisha kwa wachezaji hao kupatiwa uraia wa Tanzania.

Taarifa ilisema wachezaji waliomba na walipewa kwa mujibu wa vifungu vya 9, 23 vya Sheria ya Uhamiaji, sura ya 357.

"Kwa muktadha huo, Idara ya Uhamiaji inapenda kuutaarifu umma watajwa ni raia wa Tanzania kwa Tajnisi," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Saa chache baada ya hapo, klabu ya Simba nayo ikatangaza kuandika barua kwenda idara hiyo, kuomba uraia wa wachezaji wake tisa wa kigeni.

Barua huyo iliyotumwa juzi na kusainiwa na Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, ilisema inaomba wachezaji wake tisa wa kigeni wapatiwe uraia ili wafanye kazi kama Watanzania.

"Sababu ya maombi haya ni wachezaji hao bado ni vijana, hivyo wana muda mrefu wa kuitumikia Tanzania, zaidi wanaweza kuwa chachu ya maendeleo ya mpira wa miguu nchini," ilieleza barua hiyo.

Ina maana hata klabu ya Simba inaona kama ni vigezo ambavyo wachezaji wa Singida Black Stars wamevitimiza na kupewa uraia, basi wachezaji wao hawawezi kuvikosa.

Turudi sasa kwenye mada yenyewe. Tujiulize, hivi ni kweli wachezaji hawa wamebadilishwa kwa sababu ya kuisaidia Tanzania, labda kwenye kikosi cha timu ya taifa (Taifa Stars), hapo baadye?

Hivi ni kweli wachezaji hawa wana uwezo wa hali ya juu mno wa kuweza kuisaidia Stars kuliko hawaliopo? Maana kuna kipengele cha kuwapa uraia watu ambao ni wataalam wa hali ya juu na vipaji vikubwa visivyo na shaka hata kidogo.

Tunaendelea kujiuliza. Je, ina maana Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Hemed Morocco, ameomba wachezaji hawa wajumuishwe kwenye kikosi hicho baada ya kujidhihirisha wana vipaji maalum?

Kama si hivyo, Morocco asiporidhika nao na kutowaita kwenye kikosi cha Taifa Stars, watanyang'anywa uraia? Tuna uhakika mpaka kufikia Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) na AFCON, wachezaji hawa watakuwa katika kiwango kinachotakiwa cha kuichezea Stars.

Je, suala hili kweli limefanywa kwa ajili ya manufaa ya taifa au klabu ya Singida Black Stars? Kwa nini wachezaji walioomba uraia wawe kutoka klabu moja tu? Binafsi zipingi wachezaji kuomba na kupewa uraia. Lakini 'uspesho' na uharaka huu ndio unaowashangazwa wadau wa soka nchini.

Angalau angepewa mtu kama Bernard Morrison ambaye amekuwa akihangaika usiku na mchana kuomba uraia bila mafanikio wengi wangeweza kuelewa kwa sababu mashabiki wa soka wanajua kiwango chake. Ni mmoja ya wachezaji wenye kipaji cha hali ya juu mno, ambaye hata angepewa hakuna ambaye angeshangaa. Huyu mmoja tu anaweza kukibadilisha kikosi cha wachezaji 11 uwanjani kikawa moto, kutokana na uwezo wake wa kuwachanganya mabeki, akili na kasi, chenga za maudhi, hivyo nchi inaweza kunufaika na kipaji chake.

Kwa vyovyote vile, mlango huu ambao umefunguliwa unaweza kuleta shida baadaye, kwa sababu tunaweza kusikia Yanga, Azam, Tabora United, Coastal Union, nao wakaomba uraia kwa wachezaji wake kwa kipengele kile kile cha Tajnisi.

Na watasema ni kwa ajili ya manufaa ya taifa, lakini kumbe ni klabu zao na wachezaji wengi wa kigeni katika kikosi kwa kisingizio hicho.

Ifike wakati siasa iachwe kwenye soka, wachezaji wapate uraia kwa manufaa kweli ya nchi na isionekane kweli ni kwa ajili hiyo, siyo kuzisaidia klabu na kusingizia nchi.

# ‘Acheni kunyanyapaa watu wenye ulemavu’

**Na Vitus Audax,** MWANZA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, amewataka watumishi wa umma kutowanyanyapaa watu wenye ulemavu, bali wahakikishe wanatoa huduma stahiki kwao.

Katambi alitoa agizo hilo juzi, jijini Mwanza, kwa maofisa ustawi wa jamii pamoja na maofisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa mikoa na halmashauri wakati akifungua mafunzo ya mfumo wa kielektroniki wa taarifa na kanzidata ya watu wenye ulemavu.

Aliwataka watumishi hao kuhakikisha wanawahudumia kwa moyo na upendo, akitaja hali hiyo ya ulemavu kuwa hutokea pasipo kuomba wala kutegemea.

Katambi aliwataka maofisa hao kutumia mafunzo waliyopatiwa katika kulisaidia kundi hilo nchini.

“Kwa kufanya hivyo mnakwenda kuisaidia jamii, wewe kama mtaalamu ukiwasaidia watu kutoka kwenye ulemavu wa asilimia 70 au 100 na akawa sawa, hata kwa asilimia 15, wewe una mchango mkubwa, hivyo hii kazi tufanye kwa moyo wa dhati, tuweze kuwahudumia,” alisema Katambi.

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Ofisa Mipango Mkoa, Henry Mwaijega, alisema idadi ya wenye ulemavu mkoani humo ni watu 10,896 ambapo kati ya hao, wenye ulemavu wa viungo ni 5,362 wasioona 1,416, wenye uoni hafifu 1,862.

Alisema wenye matatizo ya afya ya akili ni 2,004 na mwenye ualbino ni 609 hivyo, ili kuhakikisha wanakuwa katika hali ya usawa, wamefanya ujenzi wa madarasa na ugawaji wa vifaa muhimu kwa wahitaji hao.

“Zaidi ya losheni 13,611 zimegawiwa kwa wenye ualbino kwa mwaka 2022 hadi 2024, ujenzi wa madarasa mawili kwa kushirikana na mdau Desk and Chair Foundation ili kuwawezesha wanafunzi kujifunzia zaidi, viti mwendo 52 kwa watu wenye ulemavu na fimbo nyeupe 70 kwa wasioona,” alisema Mwaijega.

# Mgombea AUC aanika vipaumbele sita

**Na Christina Mwakangale**

MGOMBEA wa nafasi ya uenyekiti Tume ya Umoja wa Afrika (AUC), Mahmoud Ali Youssouf, amesema iwapo atachaguliwa vipaumbele vyake vitajikita maeneo sita.

Maeneo hayo ni pamoja na uwekezaji kwenye teknolojia kurahisisha upatikanaji mtandao na bei nafuu hadi vijijini barani Afrika.

Youssouf, ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa Djibouti, amesema katika siku 100 ofisini atazingatia pia, vipaumbele vingine ambavyo ni kilimo, uchumi, afya, miundombinu, ili kuliondoa bara hilo kwenye utegemezi wa kiuchumi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, jijini Dar es Salaam, alisema anawania nafasi hiyo pamoja na wagombea wengine kutoka nchi ya Kenya na Madagascar, akieleza kwamba anafaa kutokana na uzoefu wake kidiplomasia.

“Nitazibadili changamoto kuwa fursa. Nina uzoefu wa kutosha kutokana na uzoefu nilionao. Nikishinda nitawezesha upatikanaji wa intaneti na wa bei rahisi hadi vijijini, ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya kiteknolojia duniani.

“Kunahitajika kuzuia migogoro, huko Libya, DRC (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo), Sudan, Sahel, pamoja na mimi binafsi nitazingatia hilo, nitahakikisha eneo la kulinda amani na kuitunza linafanya kazi,” alisema.

Alisema Bara la Afrika linahitaji jeshi imara, ili inapotokea dharura lifanye kazi na kwamba usalama wa bara hilo, kutawezesha kufikia lengo la Afrika tuitakayo ifikapo 2063.

Kwa upande wa kilimo, alisema kunahitajika uwekezaji na mnyororo wa thamani wa mazao, ili malighafi zinazopatikana zilinufaishe bara.

“Kuna vikwazo vya kiuchumi, miundombinu, mipakani, usafiri wa anga pia. Biashara zetu zinakuwa za msongamano sana hatuna usafiri wa anga wa uhakika na wa kutosha.

“Kunahitajika uchumi wa kikanda wa pamoja. Tuna nguvu ya kutoka barani ambako asilimia takribani 60 ni vijana. Kwenye mabadiliko ya tabianchi tunahitaji sauti ya pamoja katika uwakilishi ili kufikisha ujumbe wetu duniani,” alisema Youssouf.

Kuhusu uwakilishi wa wanawake kwenye nafasi za uamuzi, Youssouf alisema ni muhimu hivyo atakaposhinda atazingatia jinsia, huku akisisitiza Afrika ijayo ni ambayo iko huru kwenye eneo la afya, hasa kuwa na uzalishaji wa dawa na chanjo.

Umoja wa Afrika (AU), ulitoa majina ya wagombea wanne wanaowania uenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AUC).

Wagombea walioidhinishwa ni kutoka mataifa ya Afrika ikiwa ni pamoja na Kenya, Djibouti, Mauritania na Madagascar.

Nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACO, zimepewa nafasi ya kutoa mrithi wa mwenyekiti wa sasa Mousa Faki, raia wa Chad, ambaye amekuwa akishikilia wadhifa huo tangu mwaka 2017.

Uchaguzi wa AUC umepangwa kufanyika mwezi ujao wakati wa Mkutano wa AU.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na wenye ulemavu), Patrobas Katambi (kulia), akizungumza na maofisa ustawi wa jamii na TEHAMA wa Halmashauri za mikoa ya Mwanza, Kagera, Geita, Simiyu, Shinyanga na Mara, wakati wa uzinduzi wa mfumo wa kielektroniki wa Taarifa na Kanzidata ya Watu wenye Ulemavu (PD-MIS), jijini Mwanza, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wahimizwa kupanga bei kwa vipimo sahihi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKULIMA nchini wametakiwa kuwa huru kupanga bei ya kuuza mazao yao ya nafaka kwa kuzingatia thamani na vipimo sahihi ili kukuza uchumi wao kwa kupata mapato ya kutosha.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Irene Mlola, katika mkutano wa wadau wa mazao ya nafaka ya dengu na choroko.

Mkutano huo umelenga kuwasaidia wakulima nchini kupata bei nzuri ya mazao hayo kipindi cha msimu wa mavuno.

Irene alisema COPRA imejizatiti kuhakikisha biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko yakiwamo hayo inafanyika kwa uwazi na haki.

Pia alisema vibali vya usafirishaji vitatolewa kwa wanunuzi waliosajiliwa na walionunua mazao hayo kupitia mifumo iliyoelekezwa na serikali.

“COPRA imejizatiti kuhakikisha biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko inafanyika kwa kuzingatia haki, hivyo vibali vya usafirishaji vitatolewa kwa wanunuzi waliosajiliwa,” alisisitiza.

Alisema lengo la COPRA ni kuona kila upande kati ya mkulima na mnunuzi wananufaika kiuchumi.

Irene aliwataka wakulima na wanunuzi kutumia fursa za uwapo wa mamlaka hiyo kuhakikisha wananufaika na kilimo cha mazao hayo yanayolimwa katika ukanda huo na maeneo mengine nchini.

Alisema serikali imewekeza katika sekta ya kilimo, hivyo wakulima wanapaswa kutumia fursa hiyo kuongeza uzalishaji wa mazao hayo na kupata faida kubwa zaidi.

Mkuu wa Mkoa huo, Evans Mtambi, aliwataka wananchi kuchangamkia fursa nyingi za kiuchumi zinazotokana na mnyororo wa thamani wa mazao hayo ya dengu na choroko kupitia mifumo iliyowekwa na serikali.

Mtambi alisema uwapo wa mifumo hiyo ya stakabadhi ghalani na minada ya mazao hayo ya kidigitali itawasaidia wakulima kuuza mazao yao kwa faida.

“Kuwapo kwa mifumo ya stakabadhi ghalani kutawasaidia wakulima wa mazao hayo kuepuka kudhulumiwa katika vipimo, lakini kutachangia kupata faida,” alisema Mtambi.

Alisema mifumo hiyo itawasaidia wakulima kupata bei nzuri ya mazao yao na kuachana na ulaghai kutumia vipimo batili.

# AZAKI zakumbushwa kusaidia wenye uhitaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI shule zikifunguliwa, serikali imezitaka AZAKI kusaidia juhudi za kuwawezesha watoto wenye changamoto zinazowazuia kusoma waende shule kabla ya mwisho wa mwezi huu.

Mratibu na Msajili Msaidizi wa Asasi za Kiraia Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Aisha Chowo, alizipa jukumu hilo, hivi karibuni katika kikao cha dharura cha wadau hao na serikali.

Aliyataka mashirika kusaidiana na serikali ili watoto wenye changamoto zinazowakwamisha kwenda shuleni wawe wameingia darasani ifikapo mwishoni mwa mwezi huu.

Aisha aliwakumbusha kuwa kazi hiyo ni kutekeleza agizo la Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Wenye Mahitaji Maalum, Dorothy Gwajima, alilolitoa mwezi Desemba, mwaka jana, kwa viongozi wa AZAKI mkoani Dar es Salaam.

Aliwataka kuwa na mpango mkakati wa kila wilaya kusaidia watoto hao wenye mahitaji kuanzia sare za shule, daftari, mabegi ya shule, wafikiwe na wasaidiwe ifikapo Januari 30, mwaka huu, ili wasome wasibaki nyumbani.

Akisisitiza zaidi Katibu Tawala wa Wilaya ya Ubungo, Hassan Mkwawa, alisema ni sehemu ya kusaidia jamii na kukumbusha umuhimu wa kuendeleza maadili mema.

Aliwaambia kuwa pamoja na kuwasaidia watoto hao kwenda shule, ofisi yake inapanga kuzitembelea asasi zote wilayani humo, kuona mchango wake kudhibiti vitendo vya mmomonyoko wa maadili kama kuendeleza ushoga.

Hilda Malosha, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Ubungo, alisema wilaya hiyo ina AZAKI 127, kati ya hizo, 150 ndizo zinajishughulisha na maendeleo ya jamii, nyingine zipo kwa maslahi binafsi.

Akichangia mada katika kikao hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya SEO, inayojihusisha na uwezeshaji wananchi, Upendo Mwinchande, alipendekeza iundwe kamati ndogo itakayopokea fedha za msaada na kuandaa namna ya kuwafikia watoto hao.

Wakati huo huo, wazazi na walezi wamekumbushwa kusimamia na kuwaelekeza watoto kushiriki ibada ili kuwajengea misingi ya imani zao, kumjua na kuwa na hofu ya Mungu, ili kukabili mmomonyoko wa maadili.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Dini Duniani iliyokusanya watoto, viongozi wa serikali na wadini mbalimbali wilayani humo, Mkurugenzi wa SEO Upendo Mwinchande alisema kumcha Mungu na kujua dini ndiyo kuwa na maadili.

"Dini ni msingi wa maadili, inasisitiza amani, upendo, kupendana na kuvumiliana inakataza uhalifu na kila aina ya ukatili dhidi ya binadamu wa rika zote," alisema.

Katika sherehe hizo, SEO ilijumuika pamoja na viongozi wa serikali na wa dini kuhimiza kujenga jamii inayotumia ibada ili kulinda maadili na kujipatia maendeleo.

Sheikh Abeid Hassan kutoka Kimara Matangini Islamic Center, alipendekeza somo la dini lifundishwe shuleni kuanzia darasa la kwanza ili kumjenga mtoto kimaadili na kiimani.

Mchungaji Walter Yobu, akiwakilisha wakristo, alisema dini ziwafundishe watu kuepuka maovu, kukemea migogoro na kufarakana, kwani vinasababisha watoto wengi kukimbilia mtaani.

Siku ya Dini Duniani huadhimishwa kila Jumapili ya tatu ya Januari na lengo lake ni kukuza maelewano na amani kwa dini zote.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo (katikati), akicheza na wakazi wa Engaruka, mkoani Arusha jana, kabla ya kutangaza kuanza kwa malipo ya fidia kwa wakazi hao, wanaopisha mradi wa magadi soda. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wananchi wa Engaruka kujazwa fedha za fidia hivi karibuni

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

SERIKALI imeagiza kuwa ulipaji fidia ya Sh. bilioni 6.2 kati ya Sh. bilioni 14.48 kwa wananchi 595 wa vijiji vinne katika Kata ya Engaruka mkoani Arusha, ufanyike kabla ya Februari 15, mwaka huu.

Wananchi wanaotarajiwa kunufaika na fidia hiyo ni wa vijiji vya Engaruka Chini, Mbaash, Idonyonado na Irerendeni wilayani Monduli na wanalipwa kwa ajili ya kupisha mradi wa magadi soda.

Akizungumza na wananchi wa eneo hilo, Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Seleman Jafo, alisema fedha hizo za fidia zimetolewa ikiwa ni mkakati wa kutekeleza miradi huo wa kielelezo wenye manufaa makubwa katika kuendeleza sekta ya viwanda, kuongeza ajira, kukuza pato la taifa na uchumi kwa ujumla .

Pia aliliagiza Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) kuhakikisha ulipaji huo unatendeka kwa haki na kufuatilia malalamiko yote ya wananchi yakayojitokeza na kushughulikiwa ipasavyo, kuandaliwa kwa mipango miji itakayoruhusu ujenzi wa hoteli na huduma nyingine za jamii.

Waziri Jafo pia aliwataka wananchi kuchangamkia fursa zitakazojitokeza kupata ajira na kuendeleza biashara.

Vilevile, alilisisitiza shirika hilo kusimamia upatikanaji wa wawekezaji wenye sifa na uwezo na si wababaishaji ili mradi huo ulete manufaa kwa taifa na wananchi kwa kurahisisha upatikanaji wa malighafi hiyo nchini na kuokoa fedha nyingi za kigeni zilizokuwa zinatumika kuagiza malighafi hiyo nje ya nchi.

Aidha, aliwasisitiza wananchi kupuuza taarifa potofu ambazo zimekuwa zikienezwa na watu ambao hawaitakii mema Tanzania wakivumisha kuwa mradi utaleta athari.

Jafo alisema NDC ambao ndio watekelezaji wa mradi huo wamekabidhiwa Cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA), kutoka Baraza la Taifa la Mazingira (NEMC) kinachothibitisha kuwa uchimbaji wa magadi soda katika eneo la Engaruka hauna athari zozote za kimazingira kwa ndege aina ya flamingo ambao wapo eneo hilo.

Dk, Jafo pia alisema serikali imeweka mpango wa kukahakisha eneo la Engaruka barabara zake zinapitika pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa umeme mkubwa KV 33 kwa ajili ya kuendesha viwanda sanjari na upatikanaji wa huduma za kijamii katika sekta za elimu, afya na maji safi na salama.

Aidha, viongozi mbalimbali walioshiriki hafla hiyo walisema mradi huo uliosubiriwa kwa takribani miaka 20, utakuwa kichocheo kikubwa cha maendeleo katika eneo hilo la Engaruka, Arusha na taifa kwa ujumla.

Naye Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, alisisitiza kuwa wizara yake itashirikiana na wananchi wa wilaya za Longido na Monduli kuweka mipaka na kuwa na mipango bora ya matumizi ya ardhi katika vijiji vya Engaruka ili kuepuka migogoro.

"Wananchi wasigombanishwe na migogoro ya mipaka kati ya Wilaya za Longido na Monduli wekeni mipaka ili maendeleo yapatikane na wizara hii itatoa ushirikiano saa zote na RC Paul Makonda pale unapoona panakero tuwasiliane ili kutatua migogoro ili wananchi waishi kwa amani," alisema.

Aliwaelekeza maofisa ardhi katika wilaya za Monduli na Longido kushiriki kikamilifu katika zoezi la kurejesha mawe ya mpaka yaliyong'olewa na kupoteza utambuzi wa mpaka huo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mariam Ditopile, aliipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kufanikisha jambo hilo ambalo limekaa muda mrefu na kuagiza fidia hiyo ilipwe kwa kuzingatia usawa na haki.

Naye Makonda alisema Arusha ni moja ya mikoa yenye bahati na kadri siku zinavyosonga, mkoa huo utatoa fursa mbalimbali za maendeleo kwenye sekta za kilimo, madini na michezo.

Alisema fursa hizo zitakazosaidia wananchi kujikwamua na umaskini na alihimiza wazawa wapewe kipaumbele wakati wa utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa kwenye Mkoa wa Arusha.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati, Mkurugenzi Mwendeshaji wa NDC, Dk. Nicolaus Shombe, alisema mradi huo umechukua zaidi ya miaka 20 tangu mchakato wake ulipoanza baada ya NDC kufanya utafiti.

Alisema NDC ilibaini uwapo wa magadi soda yenye mita za ujazo bilioni 3.8 sawa na tani milioni 787 ambapo kupitia utekelezaji wake, viwanda viwili vikubwa vitakavyogharimu Sh. trilioni 1.6 vitajengwa katika eneo hilo lenye ekari 60,884.

Dk. Shombe alisema viwanda mbalimbali vinatumia magadi soda hayo na Tanzania ni waagizaji wakubwa wa bidhaa hiyo kutoka nchi za Boswana na maeneo mengine huku ikitumia fedha nyingi za kigeni kuagiza.

Alisema mradi huo unaenda kusaidia kuokoa fedha za kigeni kwani badala ya kununua nje magadi hayo yatatokea eneo la Engaruka.

Vilevile, alisema elimu ya fedha imetolewa kwa wananchi waliopo eneo hilo na kwamba wananchi watakaolipwa fidia watatakiwa kuondoka katika eneo hilo ndani ya siku 90 zijazo.

Naye Mbunge wa Monduli, Fredrick Lowassa, alisema wananchi wana nyuso za furaha kutokana na fidia hiyo na kuiomba serikali kushughulikia changamoto za miundombinu zilizopo.





# UWT yapongeza Samia kuteuliwa kugombea urais

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAWAKE wa Mkoa wa Dodoma wametoa tamko la kumpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupitishwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa mgombea wa urais kwenye uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Akisoma tamko hilo jana kwa niaba ya makundi ya wanawake, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Dodoma, Neema Majure alisema katika uongozi wake Rais Samia ameonesha uwezo kwenye miradi ya sekta ya afya, elimu, miundombinu, maji na nishati ambayo imewasukuma kutoa pongezi hiyo.

Alisema kwa kipindi kifupi cha uongozi wake amefanya kazi kubwa ambayo imeonesha mabadiliko makubwa ya maendeleo ambayo wananchi wameshuhudia.

"Rais amepunguza vifo vya wanawake na watoto kwa kujenga hospitali za rufani za wilaya, zahanati, vituo vya afya, kuwekeza kwenye vifaa tiba na kuajiri watumishi wa afya," alisema.

Aidha, alisema amewatua mzigo wa elimu wazazi kwa kutoa elimu bora, amewatua ndoo kichwani, ameleta nishati safi ya kupikia na mitungi ya gesi ya ruzuku imeanza kusambazwa.

Alisema wanawake hao wanaimani kubwa na Rais Samia na watahakikisha wanamuunga mkono kwenye uchaguzi mkuu kwa kumpa kura nyingi za heshima.

Pamoja na hayo, alisema wanampongeza Dk.Emmanuel Nchimbi kwa kupitishwa kuwa Mgombea Mwenza na Dk.Hussein Mwinyi kwa kuthibitishwa kuwa mgombea urais Zanzibar.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema Rais Samia amewapa tabasamu wanawake wa Dodoma kutokana na miradi aliyotekeleza imewagusa moja kwa moja.

"Rais Samia ni kiongozi mwenye mguso mkubwa kwa anaowaongoza ameleta tabasamu kwa wanawake, naungana nanyi kumuunga mkono kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa Watanzania," alisema.

# Serikali kuendelea kuinua uchumi kaya maskini

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene amesisitiza serikali itaendelea kuinua kipato cha kaya maskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) kukabiliana na changamoto za maisha.

Simbachawene alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wanufaika wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini wa TASAF wa Kijiji cha Kinyakae Manispaa ya Singida.

"Nilikuwa nasikiliza ule Mkutano Mkuu wa CHADEMA (Chama cha Demokrasia na Maendeleo) nikamsikia Freeman Mbowe anasema serikali ya CCM (Chama Cha Mapinduzi) inataka kuondoa umasikini wa watu kwa TASAF kwa kuwagawia hela," alisema na kusisitiza kuwa:" Nataka nimwambie ndio serikali ya CCM inataka kuondoa umasikini wa watu wake wale wasiojiweza kabisa kwa kuwasaidia fedha."

Simbachawene, aliendelea kusisitiza kuwa serikali itaendelea kuitumia TASAF kuondoa changamoto zinazogusa maisha ya wananchi moja kwa moja kwa kwenda kurekebisha miundombinu na vikwazo katika maisha yao.

**Alisema TASAF ni mojawapo ya mipango mingi inayotekelezwa na serikali nchini kuwawezesha wananchi kiuchumi kama ilivyo katika nchi nyingine duniani na kuondokana**

Alisema TASAF ni mojawapo ya mipango mingi inayotekelezwa na serikali nchini kuwawezesha wananchi kiuchumi kama ilivyo katika nchi nyingine duniani na kuondokana na umaskini. Alisema hivi karibuni serikali iliwaondoa wanufaika wa TASAF 400,000 baada ya hali zao za maisha kuwa nzuri baada ya kuanzisha miradi ya maendeleo kupitia fedha walizokuwa wakipata kupitia mpango huo wa kunusuru kaya masikini.

"Hawa 400,000 walio'graduate' (hitimu) wengine walikuwa hawana hata uwezo na hawajawahi kuwa hata na godoro, lakini sasa wana magodoro kwa hiyo TASAF inawasaidia sana watu maskini na itaendelea kufanya hivyo," alisema waziri huyo.

Alisema serikali itaendelea kuhakikisha kaya masikini zinajikwamua kiuchumi kupitia miradi inayotekelezwa na TASAF kupitia mpango huo unaotekelezwa mikoa yote nchini.

Awali, Simbachawene, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 47.9 kwa mkoa huo wa Singida kunusuru kaya masikini kwa kuanzisha miradi na kukabiliana na changamoto ndogondogo za maisha.




Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Japhet Hasunga, akizungumza na waandishi wa habari, baada ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, jijini Dodoma juzi. **PICHA: WU**

# Mradi kuondoa vijana 6,000 vijiweni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MRADI wa Rika Balehe unatarajia kuwafikia vijana zaidi ya 6,000 mkoani hapa na kuwatoa katika mazingira hatarishi vijiweni kwa kuwawezesha kujiajiri.

Hayo yalisemwa na Ofisa wa Afya ya Uzazi wa Mradi wa Ahadi, Elizabeth Kahabi wakati akitoa mafunzo kwa ushirikiano na wataalamu wa afya wa Halmashauri ya Jiji Dodoma kwa vijana wa kike na wa kiume, wazazi na walezi yaliyofanyika jana katika Kata ya Nzuguni.

Elizabeth, alisema mradi huo umelenga vijana wao wenye umri kati ya miaka 10 hadi 24 na kutekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la TAHEA.

Alisema shirika hilo limechukua hatua hiyo ili kufanya mabadiliko ya tabia kwa vijana wa rika hilo kwa kuwapa elimu ya stadi za maisha na kuanzisha miradi ya kujiinua kiuchumi na familia zao badala ya kukaa vijiweni na kujiingiza katika tabia zisizokubalika katika jamii.

Alisema kwa Dodoma, mradi huo unatekelezwa katika kata za Chamwino, Nzuguni, Nkuhungu, Kikuyu Kaskazini na Kikuyu Kusini.

Hata hivyo, alisema wakati wa utekelezaji wa mradi huo walikuwa wakikutana na changamoto kwa baadhi ya wazazi na walezi kukosa uelewa wa umuhimu wa mradi huo kwa rika hilo.

Alisema TAHEA itaendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha kupitia miradi wanayotekeleza nchini inaleta matokeo chanya kwa jamii.

Muuguzi wa Zahanati ya Mahomanyika, Diana Liakwiza, alishukuru TAHEA kwa mradi huo kwa sababu utasaidia kuwapa elimu ya uzazi wa mpango vijana wa rika hilo na kujiepusha na mimba za utotoni.

Diana, alisema mradi huo una manufaa makubwa kwa jamii kwa sababu utawaweka vijana katika hali ya kujitambua na kufahamu umuhimu wa kuzingatia njia za uzazi wa mpango.

Alex Ndama, Mkazi wa Kijiji cha Mahomanyika, aliipongeza TAHEA kwa kuanzisha mradi huo kwa kuwa utasaidia kutatua changamoto ya vijana kuacha kukaa vijiweni na kufanya kazi.

Ndama, alisema vijana wengi wamejenga tabia ya kukaa vijiweni kujdili mambo yasio ya msingi na kushindwa kutimiza ndoto zao na kujihusisha na makundi yasiofaa.





## Mv. Mapinduzi kuanza kusafirisha abiria Feb.

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MELI ya Mv. Mapinduzi inatarajia kuanza kutoa huduma ya usafiri kwa wananchi mwezi ujao baada ya matengenezo kukamilika.

Hayo yalisemwa jana na Nahodha wa Mv. Mapinduzi, Abubakar Mzee Ali baada ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum Mohamed, kufanya ziara ya kukagua meli kwenye Bandari ya Malindi ilikotia nanga kwa muda mrefu kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo ya injili baada ya kupata hitilafu.

Nahodha Ali, alisema kwa sasa meli hiyo ipo katika hatua nzuri na kilichobakia ni kufanyiwa matengenezo madogo na kuanza kutoa huduma kwa wananchi mwezi huo.

Awali Waziri huyo, alisema serikali ililazimika kuifanyia matengenezo meli hiyo namba mbili baada ya kutia nanga kwa muda mrefu kutokana na kupata hitilafu kwenye injini.

Alisema matengenezo yote makubwa yamekamilika na mafundi wameridhika kuwa meli hiyo ipo katika hali nzuri.

Alisema matengenezo hayo yamechukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa kutokana na vifaa vingi kuharibika na kuagizwa nje ya nchi.

Dk. Khalid, alisema meli hiyo imefanyiwa majaribio ya safari fupi mara tatu na mafundi wa Kampuni ya KOOKJE wa nchini Korea ya Kusini.

Alisema katikati ya mwezi ujao, meli hiyo itafanyiwa majaribio mengine ya masafa marefu kwa kuipeleka kisiwani Pemba na baadaye Cherezoni Mombasa nchini Kenya kwa ukaguzi na kufanyia matengenezo ya mwisho kisha kupakwa rangi.

Meli hiyo kabla ya kusitisha huduma, ilikuwa ikitoka safari zake katika Bahari ya Hindi ya Zanzibar, Dar es Salaam na Mtwara.

# Zanzibar kutumia umeme wa upepo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VISIWA vya Zanzibar vinatarajia kuondokana na tatizo la kukatika kwa umeme baada ya kuanza kutumia nishati hiyo inayozalishwa na upepo mwishoni mwa mwaka huu.

Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Joseph Kilangi baada ya Kampuni ya Seel Ilfild Service ya Dubai ikishirikishiriana na Kampuni ya Sany Renewable Energy ya China na Shirika na Umeme la Zanzibar (ZECO) visiwani hapa jana.

Kilangi, alisema umeme huo wa upepo utazalisha megawati 200 na kugharimu dola milioni 180 pamoja na ujenzi wa mitambo ya kisasa.

Alisema kituo cha kufua nishati ya umeme huo wa upepo kitajengwa eneo la Matemwe lililopo Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa awamu mbili.

Alisema baada ya awamu ya kwanza ya ujenzi huo kukamilika, kituo hicho kitazalisha megawati 120 kati ya hizo 100 ni kwa ajili ya matumizi ya Kisiwa cha Unguja na nyingine 20 Pemba.

"Kwa hakika wizara kupitia mradi huu tunataka uwe wa haraka zaidi na ndiyo maana ukawa wa mwaka mmoja au siku 360 na tupo tayari kushirikiana na mdau wetu huyu kuona unakamilika kwa wakati," alisema Kilangi.

Alisema dhamira serikali kusaini mkataba huo ni kupunguza utegemezi wa chanzo kimoja cha maji kuzalisha umeme na kuhakikisha unapatikana wa kutosha na endelevu kwa wananchi visiwani hapa na wenye viwanda.

**"Nikupongezeni sana baada ya kusikia kuwa kituo hiki cha mafuta kimejengwa na mafundi wenyewe wa kikosi cha Valantia kwa kushirikiana na mzabuni ambaye anahusika...**

"Wizara yetu na serikali haikukurupuka juu ya kufanya utafiti kuwapo kwa upepo kwa ajili ya kupata nguvu hizo, Zanzibar upepo upo wa kutosha kwa uzalishaji wa nishati ya umeme," alisema Kilangi.

Alisema kukamilika kwa mradi huo, kutaondoa tatizo la umeme kuwa mdogo na kukatika mara kwa mara visiwani hapa.

Kilangi, alisema Zanzibar kwa sasa ni maarufu kwa fursa za uwekezaji, utalii na biashara, hivyo ni lazima umeme uwepo wakati wote na huduma yake iwe bora.

Alisema kwa kituo cha umeme huo wa upepo kwa Pemba kitajengwa Mwambe.

"Watu wengi hawajui kuwa umeme tunaochukua Tanzania Bara umezidiwa kwa kuwa na watumiaji wengi kwa sasa ndiyo maana una changamoto ya kuwa mdogo ama kukatika mara kwa mara," alisema Kilangi.

Meneja Mkuu wa ZECO, Haji Muhamed Haji, alisema mradi huo ukikamilika, utasaidia kukuza viwanda na kuvutia zaidi wafanyabiashara kuja kuwekeza visiwani hapa.

"Tunaamini ukikamilika tu mradi huu utakuwa suluhisho la kuondokana na tatizo la umeme hapa Zanzibar na tumejipanga kutoa ushirikiano na mwenzetu huyu ili kazi ikamilike kwa wakati," alisema Haji.



Ofisa kutoka Kampuni ya Airpay, Wema Kilongola (kushoto), akiingiza taarifa za wanakikundi cha ujasiriamali kwenye mfumo wa kuomba mkopo kwa njia ya kidigitali, wenye lengo la kurahisisha uombaji na utoaji wa mikopo inayotolewa na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA), Gombani Pemba, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Unguja, Pemba waitwa kukopa kidigitali

**Na Mwandishi Wetu,**
PEMBA

WAKAZI wa visiwa vya Unguja na Pemba, wametakiwa kuchangamkia mikopo kwa njia ya kidijitali baada ya kuanza kutolewa na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar (ZEEA) kukabiliana na umaskini kwa kuanzisha biashara.

Rai hiyo ilitolewa jana na Ofisa Mikopo wa ZEEA, Suleiman Ali Hamad wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa maofisa mbalimbali wakiwamo wa serikali yaliyofanyika Gombani Pemba.

Hamad, alisema fomu za maombi ya mikopo hiyo zitatolewa mtandaoni na sio kwa kutumia makaratasi ili kurahisisha wananchi kupata fedha kwa wakati.

"Mikopo itaanza kutolewa kidijitali, leo hapa watu wanaendelea kupatiwa mafunzo ambayo ni muhimu kuhakikisha wanafanikiwa kuomba mikopo hii kwa njia ya mtandao, tunaamini hawa wanaopata mafunzo watakwenda kuwafundisha na wengine," alisema.

Mratibu wa ZEEA Ofisi ya Pemba, Haji Mohamed Haji, alitaja baadhi ya masharti ya kuomba mikopo hiyo kwa njia ya mtandao kuwa ni lazima kikundi kisajiliwe na kitambulisho cha Mzanzibari Mkazi.

Ofisa Akiba na Mikopo Idara ya Maendeleo ya Ushirika Pemba, Zuwena Abdalla Suleiman, aliwataka viongozi wanaposajili vikundi kuwa na sifa.

"Ikitokea mmoja wa kiongozi amekosa sifa kikundi kinatakiwa kubadilisha Katiba kwa kumbadilisha kiongozi huyo, ndio maana tumekuwa tukitoa elimu ya kuhakikisha kila mtu anakuwa na vigezo vyote ikiwamo kitambulisho cha Mzanzibari Mkazi," alisema.

Ofisa Kitengo cha Fedha Jumuishi wa Kampuni ya Airpay Tanzania, Majid Makilla, alisema wamejipanga kuhakikisha mfumo huo wa ZEEA wa kutoa mikopo kwa Wazanzibari upo sawa muda wote ili kuruhusu waombaji kupata fedha kwa wakati.

Ofisa Mikopo na Mauzo wa Benki ya Taifa ya Biashara (TCB), Khamis Juma Khamis, alisema mfumo huo utaweka uwazi na kuwataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo ili kupata mikopo.



GIGY MONEY AMCHOKOZA ZUCHU

Ukurasa 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT

JUMAMOSI JANUARI 25, 2025



# TUTARAJIE ZAIDI YA HAYA

PENGINE kinachoonekana ukaribu wa mwanamuziki wa Marekani, Travis Scott na msanii wa Tanzania, Diamond Platnumz, watu watarajie chochote kinaweza kutokea kuanzia sasa.

Diamond ni miongoni mwa wanamuziki wachache Afrika ambao wanatumia vyema fursa ya kuwa karibu na wanamuziki wa Marekani, ikiwa kufanya nao kolabo.

Hivi karibuni, rapa huyo maarufu alionekana akicheza kibao maarufu cha Diamond, 'Komasava' akiwa katika klabu moja ya usiku katika jiji la Paris nchini Ufaransa.

Video hiyo ambayo inamwonyesha Scott akifurahia wimbo huo ni uthibitisho wawili hao wana ukaribu ambao unaweza kutoa jambo la kushangaza.




# Chris Brown hataki utani

MWANAMUZIKI wa Marekani Chris Brown, amefungua kesi ya dola milioni 500 dhidi ya kampuni ya Warner Bros, akidai kukashifiwa na kufadhaika kihisia kutokana na makala zinazomwonyesha kama mnyanyasaji.

Makala hizo ambazo zilitolewa mwishoni mwa 2024, zilirudia tukio la shambulio la Brown la 2009 dhidi ya Rihanna na matukio mengine yanayodaiwa kuhusisha unyanyasaji dhidi ya wanawake.

Brown, kupitia timu yake ya wanasheria, anaeleza kwamba filamu hiyo inamwakilisha vibaya mteja wao katika matukio yanayojumuisha maelezo ya uwongo yaliyoundwa ili kuharibu sifa yake.



## Scott atoa mkono wa pole

RAPA maarufu wa Marekani, Travis Scott, ametangaza kutumia mauzo ya wimbo wake mpya 4X4, kuwachangia watu walioathirika na janga la moto Los Angeles.

Inaelezwa kuwa huenda mchango wa Scott ukawa miongoni mwa michango mikubwa zaidi kutolewa kwa waathirika wa moto.

Mchango huo wa Scott, unakuja siku chache tangu mpenzi wake wa zamani Kylie Jenner ambaye ni mdogo wa Kim Kardashian kutoa msaada mkubwa kwa waathirika hao.

## Odumo eti pesa kwake sio chochote

MSANII wa Hip hop kutoka Nigeria, Odumodublvck amesema katika maisha yake pesa na umaarufu sio muhimu kwake.

Rapa huyo alieleza kuwa ingawa anafanya kazi kwa bidii ili kujitangaza na kupata pesa, yeye hajali sana kwani anachothamini ni uhalisi na kuishi kawaida.

"Nataka niweke wazi ili watu wanisikie, kuna baadhi ya watu ukiwapa pesa na umaarufu, afadhali wasiwe na chochote na ndivyo nilivyo mimi napenda maisha rahisi pesa sio muhimu kwangu," amesema.





## Joeboy akumbuka utotoni

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria Joeboy, amesema ameanzisha taasisi yake ya kuwalipia ada za shule kwa watoto masikini kutokana na maisha magumu ya utotoni aliyopitia.

Akizungumza hivi karibuni, mwimbaji huyo alikumbuka jinsi alivyorudishwa nyumbani mara kwa mara kutokana na kukosa karo ya shule na ilimbidi kufanya biashara ili kupata pesa za kwenda kulipa.

"Nilipokuwa mdogo nilikuwa nadaiwa sana karo na ilikuwa inatia aibu, katibu wa shule alikuwa akija na majina ya wanaodaiwa ada, kabla hata hajaanza kutangaza darasa zima alikuja na kutaja jina langu, iliniuma sana."

## Burna Boy apiga 'mkwara'

MSANII maarufu wa muziki wa Afrobeats, Burna Boy amemwonya mwanamuziki mwenzake Speed Darlington, kuacha kumfanyia fujo kwani anaweza kuozea jela.

Darlington, ameachiliwa huru hivi karibuni baada ya kukaa mahabusi kwa muda wa miezi miwili kwa makosa ya kukiuka sheria za mtandao.

Burna Boy, kupitia ukurasa wa Istagram, amemtahadharisha msanii huyo akiendelea na tabia hiyo safari nyingine hawatamwone huruma na ataendelea kusota gerezani.





# Mhasibu kortini kwa utakatishaji fedha, uhujumu uchumi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MHASIBU Msaidizi wa Zahanati ya Endanachani ya Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, Mohamed Baya(33), amefikishwa mahakamani kujibu mashtaka 52 ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi na kusababisha hasara ya Sh. milioni 48.09 mali ya serikali.

Mshtakiwa huyo alifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Babati jana na kusomewa mashtaka hayo na wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Martin Makani, akisaidiana na Davis Masambu na Catherine Ngesi.

Wakili Makani, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Karimu Mushi, aliyataja mashtaka hayo yanayomkabili mshtakiwa huyo kuwa la kwanza ni ubadhirifu na ufujaji, la pili utakatishaji fedha haramu na la tatu ni kughushi.

Alidai kuwa mashtaka mengine 49 yanafanana na shtaka la kughushi kinyume na sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Makani alidai mshtakiwa huyo anadaiwa katika kosa la kwanza kuwa alikiuka sheria ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu cha 28 (1) Aya ya 21 jedwali 1 kifungu cha 57(1) na 60(2) vya sheria ya uhujumu uchumi na makosa ya kupanga sura 200 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

**Alidai mshtakiwa huyo aliendelea kughushi nyaraka kwa nyakati tofauti na kutoa fedha kinyume na utaratibu kufikia Sh. milioni 48.09.**

Alidai Oktoba 17, mwaka 2022 akiwa Halmashauri hiyo katika Zahanati ya Endanachan akijua na kwa makusudi aliandaa nyaraka za hundi kwa lengo la kuonesha zimesainiwa na watia saini ili kwenda kutoa Shilingi milioni 1.5 benki.

Makani, alidai mshtakiwa huyo akiwa na nyaraka zisizo halali, aliandaa hundi yenye namba 000182 Septemba 17, mwaka 2022 na kutoa Shilingi milioni 1.2 benki bila kujali nyaraka hizo siyo sahihi.

Alidai mshtakiwa huyo aliendelea kughushi nyaraka kwa nyakati tofauti na kutoa fedha kinyume na utaratibu kufikia Sh. milioni 48.09.

Mwanasheria huyo wa TAKUKURU, alidai upelelezi wa kesi hiyo namba 2081 ya mwaka huu ya uhujumu uchumi umekamilika na kuomba ipangwe ndani ya siku 14 ili kusikiliza hoja za awali.

Aliiomba mahakama hiyo kumnyima dhamana mshtakiwa huyo kwa kuwa kesi hiyo ya uhujumu uchumi, inayomkabili haina dhamana.

Mshtakiwa huyo alikana mashtaka hayo na kesi hiyo kuahirishwa mpaka Februari 5, mwaka huu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Hakimu Mushi, aliamuru mshtakiwa huyo kurudishwa rumande kwa kuwa mashtaka hayo yanayomkabili hayana dhamana, kwa mujibu wa sheria.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Jumaa Mhina (katikati), akizungumza wakati akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi la Mapendekezo ya Mpango wa Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026, wilayani humo, juzi. Wengine ni Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) wa mkoa huo, Stratton Lufyagila (kulia), Katibu Nyenza Adam (wa pili kulia), Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWA) wa mkoa huo, Athumani Kayumba (wa pili kushoto) na Kaimu Katibu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) wa mkoa huo, Penina Mkunduge. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Loliondo kupata maji 'bwerere'

**Na Allan Isack,** NGORONGORO

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Arusha imeongeza kiwango cha upatikanaji maji kwa wananchi kwa kujenga tangi la maji lenye ujazo wa lita 300,000 na mtandao wa mabomba wenye urefu wa zaidi ya kilomita 30 hadi kwenye makazi yao.

Maji hayo yanasambazwa kwa wananchi hao wanaoishi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Loliondo na vijiji jirani, ikiwamo vya Lopoluni na Oldonyowasi.

Kwa mujibu wa Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Ngorongoro, Gerald Andrew, mradi huo, ukamilikaji wake umefikia asilimia 85.

Andrew, alisema mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano wa serikali na wadau wa maendeleo kutoka Falme za Kiarabu.

"Mradi huu, tunatarajia utakamilika hivi karibuni na utasaidia kupunguza adha ya maji waliyokuwa wanaipata wananchi kwa miaka mingi kwa kuwa walikuwa wanatembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma ya maji," alisema.

# Makonda awapigia debe vijana Kimasai waajiriwe 'magadi soda'

**Na Godfrey Mushi,** MONDULI

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda ameagiza kipaumbele cha kwanza cha ajira katika mradi wa uwekezaji wa madini ya 'magadi soda' wa Engaruka wilayani hapa kwa vijana wasomi wa jamii ya wafugaji ya Wamaasai ili wajikwamue kiuchumi.

Makonda alitoa agizo hilo jana wilayani hapa wakati serikali ilipokwenda kuanza kulipa fidia ya zaidi ya Sh. bilioni 14 kwa wananchi 599 wanaomiliki ardhi katika vijiji vinne kupisha utekelezaji wa mradi huo wa kimkakati baada ya kukwama kwa zaidi ya miaka 20 kuzalisha madini hayo ya asili katika Bonde la Engaruka.

"Ajira kwa vijana wetu kumekuwa na kilio kikubwa. Ndugu zangu Wamaasai wengi wamesoma, lakini hawapati ajira. Mheshimiwa Jafo (Seleman Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara) na katibu mkuu wako (Hashili Abdallah), utaratibu wa huu mkoa una baba wake na mimi ndio baba wa huu mkoa," alisema Makonda na kuongeza kuwa:

"Local Content (wazawa kupata ajira na kunufaika na miradi), ndio kipaumbele. Usione watu wamepiga rubega, wana degree hapa. Mnatuchukulia poa sana nyie mnaovaa suti, lakini sisi na rubega zetu tuna degree (shahada ya kwanza) na masters (shahada ya umahiri) zetu.

... hakikisha hakuna kijana anaachwa nyuma, elimu ipo, uaminifu upo, uadilifu upo na uwezo wa kuchapa kazi upo. Wanufaika wa miradi waanze kuwa vijana wa mkoa wetu."

Kazi hiyo ya ulipaji fidia kwenye eneo hilo zaidi ya ekeari 60,800 ilizinduliwa na Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Seleman Jafo.

Akizungumza katika eneo hilo, Jafo, alisema kutekelezwa kwa mradi huo kutainua kwa kiwango kikubwa uchumi wa nchi.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), Dk. Nicholaus Shombe, alisema mradi huo uliasisiwa mwaka 1999 na kukumbana na vikwazo kutoka kwa wanaharakati wa mazingira wa nje ya nchi kwa madai ungeharibu mazalia ya ndege aina ya Flamingo katika Ziwa Natron.

Shombe, alisema umefanyika usanifu mpya mbali kabisa na ziwa hilo lililopo Bonde la Engaruka lililopo wilayani hapa.

## TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Disco la zamani, spika moja juu mtini, nyingine kwenye mtungi

**Na Adam Fungamwango**






MAISHA yanakwenda kasi sana. Hivi sasa disco linatumia vyombo vingi vya kisasa, muziki ukipigwa unaweza kusema kuwa labda kuna dansi linapigwa laivu.

Kwa sasa kuna vyombo ambavyo vinafanya muziki uwe na sauti kubwa zaidi na nzito, kiasi kwamba unaweza hata kukuzibua masikio.

Disco la sasa liwe kwenye kumbi za starehe, harusi, ubatizo, kipaimara ya sherehe zingine za kijamii, linaweza kupigwa sehemu lakini watu waliokuwa kilometa nyingi mbali wakasikia.

Ni kwa sababu ya teknolojia kuzidi kukua. Kila kukicha wataalamu wanatengeneza vyombo ambavyo vitaufanya muziki uvutie zaidi. Ndiyo maana zamani muziki ulikuwa uko kwenye mfumo wa mono, lakini baadaye wataalamu wakatengeneza vifaa ambavyo muziki ukawa unasikika kwenye mfumo wa stereo.

Mono ni mfumo wa sauti ambayo inasikika bila kuchujwa. Kama ni muziki unasikika jinsi ulivyo bila sikio kuchambua kama kuna vyombo gani vinapigwa, au sauti.

Mfumo wa stereo inaonyesha sauti iliyochujwa. Wanamuziki wenyewe wana msemo wao kuwa 'imeondolewa mafua' Sauti ya mono wanaiita yenye mafua. Hata muziki ukisikika kwa mfumo wa stereo msikilizaji atasikia sauti nyororo, na vyombo vilivyotumika vikijipambanua na kusikika vizuri kabisa.

Wataalamu siku zote hawalali. Wakaendelea kuumiza kichwa ndipo walipogundua kuongeza vifaa vya kuongeza sauti kama vile 'booster Amplifier', 'subwoofer amplifier', na vingine vingi vinavyofanana na hivyo.

Hata redio za kisasa maarufu kama 'sabufa' zina sauti kubwa, nzuri, zilizochujwa na mpangilio mzuri wa besi, kiasi cha kuweza hata kuchezesha disco.

Zamani haikuwa hivyo. Ni kweli vyombo vya muziki vilikuwa na sauti, lakini hazikuwa na mfumo mzuri kwenye mpangilio au mfumo wa besi.

Sasa hebu tuhame na kurudi miaka mingi nyuma ambapo watu walipokuwa wakitaka kufanya sherehe za kijamii, iwe za kumaliza shule, chuo, harusi, au disco tu la kawaida.

Achana na zile disco za kwenye kumbi. Nalozungumzia mimi ni lile la mitaani na vijijini.

Mashine moja ya muziki maarufu wakati huo kikiitwa 'record Player', ndiyo iliyokuwa inatumika.

Ni kitu mfano wa sanduku ambacho kilikuwa kinazungusha santuri iliyorekodiwa na bendi mbalimbali za muziki. Sanduku hilo lilikuwa likifunikwa na spika zake mbili.

Zile spika zilikuwa na sauti, lakini zilikuwa na stereo sana, lakini hazikuwa na besi.

Kama muziki unasikilizia nyumbani wala haikuwa na tatizo. Lakini kama ni sherehe na hakukuwa na chombo kingine cha kuweza kupiga disco, basi 'player' ilifanyiwa utaratibu itoe sauti kubwa zaidi ya ila ya kawaida.

Hapo ndipo utatafutwa mtungi mkubwa, na kile kisanduku cha spika ya kwanza ikawekwa ama juu ya mtungi au ndani, itategemea na mtaalamu mwenyewe atakavyoweza kuiseti.

Lengo hapo ni kupata mdundo wa besi ili kunogesha au kupata ladha halisi ya wimbo, pamoja na kuweza kuchezeka kwa raha.

Muziki bila besi ni kama chakula bila chumvi, ndimu, pilipili au kachumbari. Na kweli spika ikiingizwa kwenye mtungi na muziki ukianza kupigwa sauti ya besi inasikika kutokana na sauti ya muziki kuzongwa mtungini.

Kuna 'player' zenye spika moja, lakini pia zipo ambazo zina spika mbili. Sasa hizi moja itawekwa kwenye mtungi na nyingine juu ya mti.

Ile inayowekwa juu ya mti lengo lake ni kwamba wote waliokuwa hapo wausikie muziki. Ikikaa chini na kwa vile kuna mkusanyiko wa watu, basi watu wa pande zikingine hawatausikia vizuri.

Spika inapandishwa juu ya mti, inafungwa, disco linaanza. Sababu nyingine watu wa mbali kidogo nao waonje ladha ya muziki wa kwenye disco hilo.

Hayo ndiyo yalikuwa na mahesabu, ufundi na ujanja wa vijana wa miaka ya 1960, 1970, 1980, hadi 1990 mwanzoni.

Hili sasa ndiyo lilikuwa linaitwa 'disco vumbi'. Maana watu kutoka sehemu mbalimbali au vijiji mbalimbali walimiminika kujuika kwenye sherehe hizo. Wanapotoka hapo ni vumbi tu mtindo mmoja, miguuni, kichwani hadi kwenye kope.

Ilipofika katikati ya miaka ya 1990, redio kaseti kubwa, zenye maspika makubwa zilianza kuingia nchini na kuchukua nafasi ya 'player'. Zenyewe sasa zilikuwa na sauti kubwa zaidi. Ziliboreshwa na kuwa na besi, pamoja na vifaa vya kuchuja sauti na kutaka kuifanya vyovyote unavyotaka.

Hapa ndipo yalipokuja mageuzi ya kutoka kwenye 'record player' hadi kwenye redio kaseti.

Na hata mauzo ya santuli yalianza kupungua, kwani watu walinunua kanda za kaseti badala yake.

Kila mwenye pesa sasa alitaka kumiliki redio kaseti badala ya 'player'.

Hata hizo redio kaseti zenyewe muda wake ulipokwisha watu waliziweka pembeni na kifaa kinachoitwa 'music system' kilianza kuchukua nafasi yake. Mpaka sasa redio za aina hiyo zipo. Ila 'subwoofer', maarufu kama 'sabufa' nazo kwa sasa zipo kwenye chati.

Kwenye disco mitaani kwa sasa zinasimamishwa spika kubwa na Ma-DJ wa kisasa wana mashine maalum za kupigia disco, na wengine wana kompyuta mpakato maarufu kama 'laptop' ambazo wanakuwa wamezihifadhi nyimbo zao. Disco likipigwa hadi mtaa wa 12 wanasikia.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Rais Tshisekedi aitisha kikao cha dharura kujadili waasi M23

**KINSHASA,** DRC

WAKATI waasi wa M23 wanaendelea kukamata maeneo ya mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Rais Felix Tshisekedi, ameitisha kikao cha dharura kujadili hali ya usalama wa nchi hiyo.

Rais Tshisekedi alikatiza ziara yake nchini Uswisi, ambako alikuwa akihudhuria Kongamano la Kiuchumi Ulimwenguni mjini Davos na kurudi nchini mwake jioni ya juzi kwa ajili ya kikao hicho.

Mkutano huo wa dharura wa usalama ulijadili kuhusu kuongezeka kwa maeneo yaliyotekwa na waasi katika mkoa wa Kivu Kaskazini.

Miongoni mwa waliohudhuria mkutano huo ni pamoja na Waziri Mkuu Judith Suminwa, mawaziri wa ulinzi na usalama wa taifa. Taarifa kutoka ikulu, ilisema Rais Tshisekedi aliitisha mkutano wa baraza kuu la ulinzi jana, na kufuatiwa na ule wa baraza la mawaziri. Baada ya vikao hivyo, inatarajiwa kutangazwa maagizo muhimu kuilinda nchi hiyo.

**MATAIFA YA MAGHARIBI**

Ubalozi wa Marekani nchini DRC, ulionya kuhusu kuongezeka kwa makali ya vita karibu na mji wa Sake na kuwashauri raia wa Marekani katika jimbo la Kivu Kaskazini wachukuwe tahadhari.

Uingereza pia ilisema waasi wa M23 walikuwa wanaudhibiti mji wa Sake na ikawataka raia wake kuondoka mji wa Goma.

Taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje ya Ujerumani pia iliwatahadharisha raia wake dhidi ya safari zote zisizo za lazima kwenda DRC.

**WASIWASI WA GUTERRES**

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, kupitia msemaji wake, Stephane Dujarric, alisema amesikitishwa na kuanza tena kwa uhasama.

Guterres aliongeza kuwa mashambulizi hayo yalikuwa na athari mbaya kwa raia na pia yanaongeza hatari ya kutokea vita vya kikanda.

Alitoa wito wa ghasia hizo kukomeshwa mara moja na kuwataka waasi wa M23 kuondoka kwenye mji wa Sake, ulioko umbali kilomita 27 magharibi mwa mji wa Goma.

Guterres pia aliwataka waasi wa M23 kuheshimu hatua ya usitishaji mapigano na kwamba alikuwa anaunga mkono juhudi za upatanishi zinazofanywa na Rais wa Angola.

**UTURUKI YATAKA USULUHISHI**

Rais Recep Erdogan wa Uturuki alitoa pendekezo la usuluhishi wakati wa alipozungumza na Rais Paul Kagame wa Rwanda ambaye yuko kwenye ziara nchini humo.

"Uturuki iko tayari kutoa msaada wowote muhimu ili kutatua mgogoro kati ya Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo," alisema Erdogan.

Rais huyo wa Uturuki ana uhusiano mzuri na Rais Tshisekedi, ambaye amefanya ziara mara mbili nchini Uturuki na Erdogan aliizuru DRC mnamo Februari 2022.

**DW**



Watoto wakipambana kupata chakula kinachogawiwa kwa Wapalestina waliokimbia mashambulizi ya jeshi la Israel katika eneo la Khan Yunis, kusini mwa Ukanda wa Gaza. **PICHA: ALLIANCE**

## Jaji Mkuu Kenya aondolewa ulinzi

**NAIROBI,** KENYA

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Kenya, imeondoa ulinzi kwa Jaji Mkuu, Martha Koome na kupunguza polisi wanaomlinda akiwa mahakamani.

Hatua hiyo imeibua mgogoro kati ya Mahakama na Serikali, huku ikielezwa kwamba polisi waliokuwa wakilinda Jaji Koome wameamriwa kuondoka na idadi ya waliokuwa katika kitengo kipya cha Ulinzi wa Mahakama imepunguzwa.

Jaji Koome alimwandikia barua Waziri wa Usalama wa Ndani, Kipchumba Murkomen na IGP wa Kenya, Douglas Kanja, kueleza hatua hiyo ni tishio dhidi ya uhuru wa Mahakama.

Koome alisema kuwa kuondolewa kwa ulinzi ni njama ya kudhoofisha ofisi hiyo ya kikatiba au ni tukio la kulipiza kisasi.

"Nina wasiwasi mkubwa kuhusu kuondolewa kwa ulinzi wa Jaji Mkuu, kitendo kinachodhoofisha uhuru wa mahakama, kinatishia heshima ya taasisi, na kuhatarisha maendeleo ya kidemokrasia. Kuondolewa kwa ulinzi huu ni kitendo cha kutukana kanuni ya mgawanyo wa madaraka," aliandika Koome.

Hata hivyo Ofisi ya Huduma ya Polisi NPS imekanusha kuondoa ulinzi, ikisema polisi walirudi jeshini kwa ajili ya mafunzo.

Msemaji wa NPS, Resila Onyango, katika taarifa yake fupi, alisema huduma hiyo inajitolea katika ushirikiano wa taasisi nyingi na kushirikiana ndani ya mfumo wa haki za jinai wa nchi.

# Rais Trump ataka bei ya mafuta kupungua

**DAVOS,** SWISS

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amezitaka nchi zinazouza petroli kwa wingi duniani (OPEC), ikiongozwa na Saudi Arabia, kupunguza bei ya mafuta.

Katika hotuba yake katika Kongamano la Kimataifa la Kiuchumi la Davos, nchini Uswisi, Rais Trump alisema bei ya mafuta iko juu na inasaidia kufadhili vita vya kati ya Russia na Ukraine.

Bei ya mafuta ghafi ilishuka kwa asilimia moja baada ya Trump kutoa kauli hiyo.

Rais Trump pia alisema atamuomba Mfalme Mohammed bin Salman kuongeza uwekezaji wa Saudi Arabia nchini Marekani hadi dola trilioni moja.

Aidha, alisisitiza kuwa serikali zote duniani zinapaswa kutengeneza bidhaa zao Marekani ili kuepuka kodi kubwa, na alitaka kupunguzwa kwa viwango vya riba ili kukabiliana na matatizo ya kiuchumi anayodai yaliletwa na utawala wa Rais Biden.

Akizungumzia matumizi ya makaa ya mawe kwa ajili ya nishati, alisema Marekani inahitaji nishati zaidi kwa ajili ya maendeleo ya akili mnemba. Wakati huo huo, Rais Trump ametia saini amri ya kuruhusu kutolewa nyaraka zinazoelezea kuhusu kuuawa kwa Rais John F Kennedy, kaka yake Bobby Kennedy na mwanaharakati mashuhuri Martin Luther King.

Agizo hilo linataka maofisa wa serikali kuwasilisha mpango wa kufichua hati hizo ndani ya siku 15. Hadi sasa, hati nyingi zinazohusiana na uchunguzi wa mauaji ya JFK na wengine zimeachiliwa, lakini maelfu bado zimefanywa siri. Bado kuna sitofahamu kuhusu kuuawa kwa kupigwa risasi kwa Rais Kennedy akiwa mjini Dallas mnamo 1963, huku kukiwa na uvumi kuwa Cuba ilihusika. Kennedy aliuawa na Lee Harvey Oswald, mstaafu wa jeshi la wanamaji ambaye alikimbilia Umoja wa Sovieti kisha alirudi tena Marekani.

Kamati ya serikali ilibaini kuwa Oswald alifanya mauaji hayo peke yake, lakini maswali ambayo hayajapata majibu yameendelea kutia shaka na kuleta nadharia kuhusika kwa maofisa wa serikali, magenge ya uhalifu na wahusika wengine.

Kwa upande wa Familia ya Martin Luther King, inadai mauaji yake yalikuwa njama iliyopangwa na serikali ya Marekani.

Rais Trump alisema sasa kila kitu kuhusu mauaji hayo, kitafichuliwa.

**BBC**

# Tanzania kuwa mwenyeji kongamano la UN Tourism

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI na Shirika la Utalii la Umoja wa Mataifa (UN Tourism) zimetia saini mkataba wa makubaliano utakaoifanya Tanzania kuwa mwenyeji wa Kongamano la Pili la Kikanda la Utalii wa Vyakula la Shirika la Umoja wa Mataifa (The 2nd UN Tourism Regional Forum on Gastronomy Tourism for Africa).

Kongamano hilo linatarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam, Machi 11 hadi 13, mwaka huu.

Hafla ya utiaji saini ilifanyika jana kati ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Pindi Chana na Katibu Mkuu wa UN Tourism, Zurab Pololikashvili, katika kikao kilichofanyika makao makuu ya shirika hilo, Madrid nchini Hispania.

Akizungumza katika hafla hiyo, Chana alisema Tanzania inafuraha kuwa mwenyeji wa kongamano hilo linalotarajia kukutanisha washiriki zaidi ya 300 kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Alisema kupitia kongamano hilo, Tanzania itajifunza kutoka mataifa hayo namna wanavyofanya katika kukuza utalii wa vyakula.

"Tunataka kuwajengea uwezo wapishi wetu namna ya kutengeneza aina tofauti za vyakula ili watalii wanapokuja waweze kufurahia vyakula vya nyumbani kwao, lakini pia tunahitaji kuona ni fursa gani zitakazotokana na kongamano hilo ili tuweze kujifunza utangazaji utalii wa vyakula," alisema.

Waziri Chana alisema Tanzania na UN Tourism zimekuwa zikishirikiana katika masuala mbalimbali kwa lengo la kukuza utalii na maeneo wanayoomba ushirikiano kwa sasa ni katika masuala ya sera na ukuzaji ujuzi, rasilimali watu na mpango mkakati wa kukuza utalii.

Alisema Tanzania inatambua na kuthamini jukumu muhimu la UN Tourism katika kuunda sera za kimataifa za utalii, kukuza utalii endelevu na kukuza ukuaji wa uchumi.

Katibu Mkuu wa UN Tourism, Pololikashvili, alisema kuwa Shirika la Utalii Duniani limelenga kuitangaza Afrika kama sehemu ya utalii inayofikika sambamba na kutangaza utalii wa vyakula.

Katika kufanikisha kongamano hilo, Pololikashvili amependekeza kwa Tanzania kutumia njia zote za mawasiliano ili kulitangaza kongamano hilo ikiwa ni pamoja na kutumia watu maarufu wenye ushawishi katika jamii na kuwatumia wapishi wa vyakula mbalimbali vya kiafrika.

"Ninaiomba Tanzania kuhakikisha mchakato wa upatikanaji wa Visa pamoja na usafiri wa anga kwa ujumla linakuwa rafiki kwa waombaji wanaotarajia kusafiri kuja kwenye kongamano hilo," alisema.

Mkutano huo umehudhuriwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania, Balozi Ramadhani Dau, Balozi wa Tanzania nchini Hispania, Balozi Ali Jabir Mwadini, Mkurugenzi wa Utalii, Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Thereza Mugobi, Mjumbe wa Bodi ya TTB, Said Kamugisha, na Ofisa Balozi, Amos Tengu na Sekretarieti ya Shirika la UN Tourism.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana (kushoto) na Katibu Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani (UN Tourism), Zurab Pololikashvili wakionyesha mkataba kuhusu Tanzania kuwa mwenyeji wa Kongamano la Pili la Kikanda la Utalii wa Vyakula la Shirika la Umoja wa Mataifa linalotarajia kufanyika mwezi Machi 11 hadi 13 mwaka huu, baada ya kutiliana saini katika Makao Makuu ya Shirika hilo, jijini Madrid, Hispania jana. **PICHA: WMU**

## PAC yaridhishwa maendeleo ujenzi uwanja Msalato

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeipongeza serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, jijini Dodoma.

Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, alitoa pongezi hiyo baada ya kutembelea na kukagua mradi huo pamoja na wajumbe wa kamati hiyo juzi.

Hasunga aliitaka TANROADS kusimamia ujenzi wa miundombinu ya kiwanja hicho ili kukamilika kwa wakati na ubora uliokusudiwa.

"Tumefurahi na tumeona maendeleo mazuri ya ujenzi wa kiwanja hiki kikubwa, tunampongeza kwa dhati Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji huu mkubwa ambao ameufanya.

"Ili kupima thamani ya fedha lazima tujue ni lini uwanja huu utakamilika na ukamilike kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa na kuanza kutumika. Tunatamani kufikia mwezi wa saba (Julai) uwe umekamilika," alisisitiza Hasunga.

Aliongeza kuwa: "Eneo la kiwanja hiki ni kubwa lenye zaidi ya ekali 11,000, hivyo litengwe eneo litakalotumika kwa ajili ya ujenzi wa hoteli, kumbi za mikutano na maduka makubwa ili kuendelea kukuza utalii na kuchangamsha uchumi wa mkoa wa Dodoma."

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Ruvuma, Jackline Ngonyani, alipongeza jitihada zinazofanywa na serikali pamoja na TANROADS kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa uwanja huo.

Awali, akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Mohamed Besta, alisema ujenzi huo umefikia asilimia 84 mpaka sasa na mkandarasi anayetekeleza mradi huo atasimamiwa kikamilifu ili ukamilike kwa wakati.

# Kliniki msaada wa sheria kutolewa bure

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MAHAKAMA Kuu Tanzania, Kanda ya Morogoro, kwa kushirikiana na taasisi 45 za kisheria zinakusudia kuweka kliniki ya msaada wa kisheria bure kwa wananchi wa mkoani hapa katika Wiki ya Sheria iliyotarajiwa kuzinduliwa Januari 25, mwaka huu.

Kaimu Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro, Stephen Magoiga, alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maadhimisho hayo.

Jaji Magoiga aliwataka wananchi kutoka wilaya zote za mkoa wa Morogoro wenye mashauri yanayohitaji msaada wa kisheria, ikiwamo migogoro ya ardhi na ile ya wakulima na wafugaji, kujitokeza kupata huduma hiyo kwenye maadhimisho hayo kupitia taasisi hizo kweye mabanda maalumu yatakayokuwa stendi ya zamani ya daladala.

Alisema maadhimisho hayo ni utekelezaji wa nguzo ya pili na tatu ya mpango mkakati wa mahakama wa upatikanaji wa haki kwa wote na kwa wakati.

Katika wiki hiyo, alisema wananchi watapata elimu ya msaada wa kisheria bure pamoja na kuwajengea uwezo juu ya utatuzi wa migogoro ya wakulima na wafugaji ili kuleta ustawi na amani nchini.

Jaji Magoiga alisema kutokana na mazingira ya Kanda ya Morogoro, wananchi wanajishughulisha na kilimo na ufugaji, hivyo wanaingiliana na kusababisha migogoro ya mara kwa mara. Alisema kutokana na hali hiyo, mahakama imeona kuna haja ya kuwasaidia wananchi kwa kuwapa elimu.

Kuhusu maadhimisho hayo kwa Kanda ya Morogoro, alisema yatanguliwa na matembezi yatakayoanzia kwenye viwanja vya Mahakama Kuu Kanda ya Morogoro hadi stendi ya zamani ya mabasi ambako kutakuwa na mabanda ya maonesho.

Alisema maadhimisho hayo yataongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Mussa Kilakala.

"Tupo kwa ajili ya kujenga imani ya wananchi na ushirikishwaji wa wadau. Mahakama ilitambua kuwa upatikanaji wa haki ni mchakato ambao unahusisha ushiriki wa wadau wa haki jinai au jinai," alisema.

Jaji Magoiga alisema mwaka 2025, Jaji Mkuu ametambulisha kaulimbinu inayohamasisha wadau wa haki madai kuhakikisha wanachangia na kushiriki katika kufanikisha azma ya serikali katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Kupitia dira hiyo, Tanzania inatarajia kuwa kati ya nchi zenye uchumi wa kati ngazi ya juu au zaidi.

Alisema mpango huo umejikita katika azma ya kuwa na taifa jumuishi lenye ustawi, haki na linalojitegemea. Dira hiyo imejengwa juu ya nguzo tatu ambazo ni uchumi imara, jumuishi na ushindani, uwezo na maendeleo ya jamii na uhifadhi wa mazingira na uhimilifu wa mabadiliko ya tabianchi.

# HADITHI

WAKATI mwingine umdhaniavyo binadamu sivyo alivyo. Unaweza kumuona ni mtu mbaya au ana roho mbaya kwa kumuangalia, lakini akawa ni mtu mzuri sana ambavyo kuhupata kudhani.
Unawezi kukutana na mtu ambaye kwa muonekano na jinsi anavyokutendea ukamuona ni mtu mwema sana. Hata hivyo ndani ya roho yake ana mambo ambayo akikifungulia unaweza kuanguka na kuzirai. Ni mtu mbaya kuliko ubaya wenyewe. Anaficha ukatili na roho yake mbaya kwa kivuli cha kujifanya mwema. Watu hawa ni hatari sana.
Kwenye kijiji kimoja kilichopo Bungu, Rufiji kunatokea mauaji ambayo hayajulikani chanzo ni nini. Mauaji hayo yanawahusisha wasichana wawili wanaosoma shule ya sekondari, pamoja na vijana kadhaa. Wananchi wanataka serikali ya kijiji ichukue hatua kwa kuwasaka wauaji ambao wakitia hofu kijiji cha Mikamba na vya jirani. Je muuaji atapatikana? Ni nani? Fuatilia mkasa huu.

# Malaika shetani-5

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




Siku moja alifuatwa na ndugu yake. Mtoto wa shangazi yake. “Kwani wewe umefanya nini mjomba?” “Kwa vipi?” “Nilipita sehemu nikasikia watu fulani wanasema tumemgundua yule alikuwa ni Feruzi. Kwa hiyo anatakiwa ashughulikiwe. Mimi sikutaka kukaa tena kusikiliza, nikakimbia kukutafuta, lakini sijakuona, leo ndiyo nakuona. Kwa hiyo mjomba kuwa makini kuna watu wanatafuta kukushughulikia.” “Du! ahsante sana mjomba Abdu kwa kuniambia hili. Nitakuwa makini kuanzia sasa.” “Kwani umefanya kosa gani?” “Ni stori ndefu, ila utaifahamu.” Akajibu Feruzi. “Mjomba isiwe ni mmoja wa watu wanaotafutwa na kumuua Naima?” Feruzi alitabasamu. Tabasamu ambalo si halisi, akamjibu “Abdu, wewe bado kijana mdogo sana, dunia hii ina mambo mengi ambayo yanahitaji upembuzi yakinifu ili kuyafahamu. Siwezi hata kuchinja kuku, achilia mbali kuua au kushiriki kumuua binadamu, ila kwenye hii dunia unaweza ukapewa hiyo kesi na ukafungwa.” Akajibu. Abdu akamwangalia mjomba wake, akamwonea huruma “Sasa unafanyaje anko?” “Hili lisikusumbue sana, mimi nitajua jinsi gani ya kudili nalo, wewe nenda nyumbani.” Feruzi hakutaka kumfafanulia mjomba wake ambaye ana umri wa miaka 15 tu. Mambo yaliyopo ni makubwa kuliko umri wake.

Akichokuwa na uhakika nacho ni kwamba aliyewasikia wakizungumza, ni watu wanaomtafuta kwa ajili ya kutaka kumuua kutokana na kuwaona siku ile alipowafuma wanataka kumfukia Naima baada ya kumuua. Hata yeye alijua hawatolala usingizi wao na waliowatuma mpaka watakapomkamata na kumuua ili kuficha ushahidi. Mpaka sasa hakuwa amemwambia mtu yeyote yule. Kitu alichosaidia baada ya kutoka pale siku ile kwa kukimbizwa ni kwenda tu kuwaambia wanakijiji kuwapo kwa mwili wa mtu. Na wanakijiji walipofika walikuta ni kama kuna watu walikuwa wanataka kuufukia lakini wameshindwa kwa kufumwa au kitu kingine kinachofanana na hicho. Feruzi hakunyanyua mdomo wake kumwambia mtu yoyote kuwa alikuta watu watatu na walimfukuza hadi alipofika karibu na kijiji cha Bungu. Kwa hiyo yeye ndiye binadamu pekee anayejua kuwa Naima ameuawa na watu watatu, ambao aliwafuma wakitaka kumfukia. Ilishindikana kwa sababu waliiacha maiti na kumfukuza. Baada ya kumkosa hawakutaka kurejea tena kwa sababu za kiusalama kwani walijua atakwenda kuwaambia wanakijiji na watafika pale haraka sana na kuwakuta.

**Kusikia bado anapendwa hata ikiwezekana ndoa ni kitu ambacho akikihitaji kwa mwanaume anayempenda ambaye ni Feruzi. “Unakwenda kutafuta maisha mjini ndugu yangu?”**

Kengele ya hatari ilianza kulia kichwani kwa Feruzi. Alijua baada ya uchunguzi wao wameshagundua kuwa yeye ndiye aliyewaona na kukimbia siku ile. Hivyo kwa usalama wa wote waliofanya tukio na walio nyuma, basi wanatakiwa wamnyamazishe. Asiongee chochote alichokiona. Hata kama tayari ameshaongea kwa mtu wau watu ambao hawawafahamu, basi kifo chake kiwatie woga wote waliosikia, wasiendelee kuzungumza. Hakuwa na raha. Alitembea kwa tahadhari kubwa. Na kweli kesho yake wakati anatembea kuelekea njia ya kisimani alisikia minong’ono kutoka kwa watu ambao hawakuonekana njiani. Kwa sababu alikuwa akiishi kimachale. Alishtuka. Akasimama, akarejea alikotoka kwa kukimbia. Alipogeuka aliona watu watano ambao walionekana walikuwa wamejificha, ama kwenye kichaka, au nyuma ya mti mkubwa uliokuwa mbele wakimsubiri kwa hamu. Ilionekana kama hawakutarajia Feruzi kuwashtukia kirahisi namna ile, ndiyo maana hawakuwa wamejiandaa kumkimbiza. Walikuwa wanamkimbiza lakini walikuwa mbali sana. Walikuwa na silaha za jadi, fimbo na mapanga na visu ambavyo alikuwa kabisa kuwa vilikuwa vimeandaliwa kummaliza.

Alikuwa na mbio kuliko walikuwa wanamkimbiza. Na kwa sababu waliomkimbiza moja ya tahadhari zao kubwa hawakutana kuonekana kama ni watu wabaya kwa wananchi, hawakufika mbali. Wakamwachia njiani huku akiwa hoi. Alifika nyumbani kwao na kuingia ndani. Ilikuwa 10:00 jioni. Giza kwa mbali lilianza kuingia. Aliona hii ni fursa adhimu ya kujiandaa kuondoka kwenye kijiji cha Bungu. Lengo ni kuondoka kukimbiza roho yake. Kuna watu wanaoitafuta.

****************************************

“Zuhura mpenzi wangu.” “Abee Feruzi, la azizi wangu.” “Leo ni siku moja kubwa mbaya sana ambayo nataka kukwambia.” Zuhura alishtuka. Pozi lake lote la kike kwa Feruzi, liliyeyuka kama kipande cha samli kwenye kikaango chenye moto mkali. “Unasemaje Faruzi?” Akauliza kwa sauti kali na ya woga, tofauti na ile ndogo, laini, yenye kubembeleza na kushawishi aliyokuwa akiongea mwanzo.

“Usishtuke sana Zuhura. Mambo haya ni ya kawaida kwenye dunia hii tunayoishi.” “We, mbona mimi leo sikuelewi? Umekunywa, au una tatizo gani?” “Wewe mwenyewe unajua kuwa mimi hunywa mara chache sana. Siyo mlevi, na ulevi wangu haujawahi kuathiri chochote kile kwenye maisha ya kawaida na mapenzi yetu.” “Sasa, mbona unan’changanya.” “Mimi nimekuita hapa nataka kukuaga.”

“Kuniaga?” Akauliza Zuhura. Bado alikuwa hajafahamu nini kinamsumbua mpenzi wake. Mwanzoni wakati anaongea akili yake ilimwambia labda anataka kulivua penzi. Lakini kwa hili analoongea, aligundua kuwa lengo siyo hilo. “Anataka kuondoka, anakwenda wapi na kufanya nini?” Akajiuliza mwenyewe. “Sina lengo baya, mimi nakupenda na nitaendelea kukupenda milele na milele. Lengo langu ni kufunga ndoa na wewe. Na kama Mungu akipenda itakuwa hivyo.” Moyo wa Zuhura kidogo ulitulia. Kusikia bado anapendwa hata ikiwezekana ndoa ni kitu ambacho akikihitaji kwa mwanaume anayempenda ambaye ni Feruzi. “Unakwenda kutafuta maisha mjini ndugu yangu?” Zuhura anauliza huku akijaribu kurejesha sauti yake tamu na laini. Lakini haikuwa kwenye ubora kama ule wa mwanzo. Walikuwa amesimama kwenye eneo moja kijijini hapo, ambako Feruzi aliona hawezi kufuatiliwa na waliomtafuta. Ni sehemu ambayo yeye aliona ni salama zaidi. Na hiki pia kiliendelea kumtisha Zuhura, ambaye awali alijua ni eneo ambalo limekaa zaidi kitulivu kwa wawili wanaopendana wakikutana. “Hapana siendi mjini kusaka maisha.” “Sasa?” “Naondoka hapa kwa ajili ya kuokoa roho yangu!” Ni jibu lililomtisha Zuhura. Kwa jinsi alivyomwona Feruzi. Awali alidhani kama ni mzaha, lakini kila akimwangalia, anaona ni mtu mwenye wasiwasi na anaongea kitu ambacho anamaanisha na si mzaha. “Kuna nini tena Feruzi mpenzi wangu?” Zuhura alimkumbatia mpenzi wake na akaanza kulia. “Usilie mpenzi. Usilie Zuhura. Wewe baki salama. Mungu akipenda nitarudi. Kuondoka kwangu hapa ndiyo usalama wangu. Kama nikikaa kwa siku moja tena mpaka kuingia kwa usiku wa kesho, sitakuwa hai. Nitaitwa marehemu. Sijui wewe, wazazi wangu, ndugu zangu mtakuwa kwenye hali gani. Kwa maana hiyo, ili niendelee kuwa hai na nyinyi mwendelee kuwa na mimi ni lazima niondoke.” “Nani anataka kukutoa uhai, na tatizo ni nini mpenzi?” Akauliza kwa Zuhura kwa kwikwi. “Ni hadithi ndefu. Ila kwa sababu wewe ndiyo mpenzi wangu na msiri wangu mkubwa nitakwambia kabla sijaondoka. Nitakwambia kwa sababu moja tu. Ili usidhani labda nakimbia au kuna sababu yoyote mbaya ya mimi na wewe nyuma ya pazia. Nawajua nyinyi wanawake mawazo yenu.”

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# WACHEZAJI 5 WAJIFUNGA WENYEWE LIGI KUU BARA

Na Adam Fungamwango

JUMLA ya wachezaji watano wamejifunga wenyewe hadi kumalizika kwa michezo ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inatarajiwa kuendelea tena kuanzia Februari, Mosi mwaka huu.

Kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya Ligi zilizotolewa jana, wachezaji waliojifunga ni Fred Tangalo wa KMC, Kelvin Kijili (Simba), Yannick Bangala (Azam) na Dickson Mhilu (Dodoma Jiji) na Jackson Shiga wa Fountain Gate ya jijini Dodoma.

Wakati takwimu za Bodi ya Ligi zikitaja idadi ya wachezaji hao waliojifunga katika harakati za kutaka kuokoa mpira isitinge wavuni, takwimu za dawati la michezo Nipashe zinabainisha, Tangalo alijifunga katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa Septemba 19, mwaka jana kwenye Uwanja wa KMC, timu yake ilipocheza dhidi ya Azam FC, na mechi hiyo ilimalizika kwa wenyeji kutandikwa mabao 4-0 katika mchezo huo.

Oktoba 19, mwaka jana, kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, wakati timu yake ya Simba ilipocheza dhidi ya Yanga, Kijili alijiunga na goli lake kuwa bao pekee katika mchezo huo.

Beki Mkongomani, Bangala wa Azam FC, alijifunga mwenyewe katika harakati za kutaka kuokoa mpira katika mchezo uliopigwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Desemba Mosi, mwaka jana, ingawa timu yake iliondoka na ushindi wa bao 3-1, huku akiwapa wenyeji bao la kufutia machozi.

Katika mchezo huo huo wa Desemba Mosi, beki wa Dodoma Jiji naye alijifunga na kuwapa Azam bao.

Ilikuwa Desemba 29, mwaka jana kwenye Uwanja wa KMC Complex wakati beki wa Fountain Gate, Shiga, naye alipojifunga katika harakati za kuokoa mpira usiingie wavuni, wakati timu hiyo ikicheza dhidi ya Yanga.

Katika mechi hiyo, Fountain Gate ilikubali kichapo cha mabao 5-0 na mpira ulipoisha tu ilimtimua kocha wake mkuu, Mohamed Muya, ambaye kwa sasa ametimkia Geita Gold, huku timu hiyo ikimchukua Mkenya, Robert Matano ambaye anasaidiwa na beki mkongwe, Amri Said.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kurejea tena kuanzia Februari Mosi, mwaka huu baada ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kutangaza kusogeza mbele Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).



Wachezaji wa Pamba Jiji FC ya Mwanza wakifanya mazoezi ili kujiandaa kuwafuata wenyeji Dodoma Jiji kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Februari 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri. **PICHA: MTANDAO**

# Tanga kuchaguana Februari 22

Na Faustine Feliciane

CHAMA cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Tanga (TRFA), kinatarajia kufanya uchaguzi wake mkuu ifikapo Februari 22, mwaka huu.

Katibu Mkuu wa TRFA, Beatrice Mgaya, aliliambia gazeti hili maandalizi ya uchaguzi huo yanaendelea vyema na nafasi zote zimepata wagombea.

Mgaya alitaja nafasi zinazowaniwa katika uchaguzi huo ni ya Mwenyekiti, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TFF (Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania) na wajumbe wawili wa Kamati ya Utendaji wa TRFA.

"Uchaguzi wetu utafanyika Februari 22. Kila kitu kinakwenda vyema na tunashukuru Kamati ya Uchaguzi inasimamia mchakato huo vizuri kwa kufuata taratibu na kanuni za uchaguzi," alisema katibu huyo.

Aliongeza uchaguzi huo unafanyika baada ya viongozi walioko madarakani kumaliza muda wao wa miaka minne.

Tayari mikoa mingine ikiwamo Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Kigoma, Rukwa, Mwanza, Katavi, Mtwara, Lindi, Kagera, Simiyu, Geita, Pwani na Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TWFA), wameshafanya uchaguzi ili kupata wawakilishi watakaoshiriki katika mkutano mkuu wa uchaguzi wa TFF utakaofanyika baadaye mwaka huu.

Uchaguzi wa mwisho wa TFF ulifanyika mwaka 2021 jijini Tanga ambapo Wallace Karia alichaguliwa kuwa Rais wakati nafasi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilikwenda kwa Athumani Nyamlani.

## KMC FC: Mapumziko yamesaidia kuimarika

Na Adam Fungamwango

UONGOZI wa KMC FC umeweka wazi mapumziko waliyopata kutokana na Ligi Kuu Tanzania Bara kusimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi na mechi za kimataifa, yamewasaidia kutengeneza kikosi chao ambacho kiko chini ya Kocha Mkuu, Kally Ongalla.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa KMC FC, Daniel Mwakasungula, alisema isingekuwa rahisi hata kidogo kwa kocha mpya (Kally), kuingiza falsafa zake na mbinu wakati michezo ya ligi ikiwa inaendelea kuchezwa.

"Kocha huyu ni mpya, alikuja na hakupata muda wa kukaa na wachezaji na kutengeneza mbinu zake, badala yake walikuwa wakitengeneza mpango mkakati wa mechi inayofuata, si rahisi kocha mpya kutengeneza timu wakati ligi inaendelea, lakini tukapata bahati tulipocheza dhidi ya Coastal Union jijini Arusha, wachezaji walipewa mapumziko ya siku nne mpaka tano hivi.

Na ilipotokea mapumziko ya CHAN (Fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani), na Kombe la Mapinduzi, kocha akaona hii ndiyo fursa, akaomba wachezaji warudi haraka ili wakitengeneze kikosi bila presha," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kutokana na kukaa muda mrefu na wachezaji kwa sasa wana matumaini na kurejea kwa kishindo katika mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

„Amepata wiki nne za kukaa na timu, na sisi viongozi tumeona maendeleo ni ya kuridhisha, yanatia moyo na matumaini yapo, na mpaka sasa tumecheza michezo sita ya kirafiki, tumeridhika na tunaamini tutarudi tukiwa bora zaidi," alisema Mwakasungula.

Hata hivyo, Bodi ya Ligi hivi karibuni ilitangaza kurudisha nyuma ratiba ya Ligi Kuu iliyokuwa irejee Machi Mosi, mwaka huu na sasa itachezwa kuanzia Februari kutokana na kuahirishwa kwa CHAN iliyokuwa ichezwe Februari Mosi hadi 28 mwaka huu hapa nchini, Uganda na Kenya, lakini imerushwa mbele hadi, Agosti mwaka huu.

Klabu hiyo ilimpa kazi, Kally, baada ya kuondoka kwa aliyekuwa Kocha Mkuu, Abdulhamid Moalin, aliyetimkia Yanga, ambapo sasa ni Mkurugenzi wa Ufundi na mmoja wa makocha wasaidizi wa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Katika msimamo wa ligi hiyo, KMC inashika nafasi ya 10 ikikusanya pointi 19 kibindoni baada ya kucheza michezo 16, ikishinda mitano, sare nne na kupoteza michezo saba.

## ZISIKUPITE

### GERNACHO ANUKIA CHELSEA

KLABU ya Chelsea inafikiria kumsajili winga wa Argentina, Alejandro Garnacho, mwenye umri wa miaka 20, baada ya Napoli kusitisha mpango wa kumsajili mchezaji huyo wa Manchester United. ***(Sky Sports)***

### CAMBIASO AIVUTIA CITY

MANCHESTER City inavutiwa na beki wa Italia, Andrea Cambiaso, mwenye umri wa miaka 24, lakini Juventus inataka kulipwa kiasi cha euro milioni 65. (***Gazzetta dello Sport***)

### DORTMUND YAKWAA KISIKI

KLABU ya Borussia Dortmund imejiondoa katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa England, Marcus Rashford, mwenye umri wa miaka 27, huku mshahara wa mchezaji huyo wa Manchester United wa pauni 350,000 kwa wiki ukionekana kikwazo. (***Mail***)

### ZINCHENKO NJIA MOJA

MLINZI wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ukraine, Oleksandr Zinchenko, mwenye umri wa miaka 28, anatarajiwa kuondoka kabla ya dirisha la uhamisho wa Januari kufungwa, huku Borussia Dortmund ikimwania nyota huyo. (***Telegraph***)

### CHILWELL KUTUA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund pia inamfuatilia beki wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell, mwenye umri wa miaka 28. (***Sun***)

### VEIGA KUONDOKA CHELSEA

CHELSEA imefikia makubaliano ya awali ya kumtoa kwa mkopo kiungo wa Timu ya Taifa ya Ureno, Renato Veiga, mwenye umri wa miaka 21, kwenda Juventus kwa muda uliosalia. (***Athletics***)

### TIERNEY KUREJEA CELTIC

MLINZI wa Arsenal na Scotland, Kieran Tierney, mwenye umri wa miaka 27, yuko mbioni kusaini mkataba wa awali wa kurejea Celtic kwa uhamisho wa bure mwishoni mwa msimu huu. (***Telegraph***)

### SILVA AKARIBIA WEST

KLABU ya West Ham inamtaka mchezaji wa RB Leipzig, Andre Silva, mwenye umri wa miaka 29, kwa mkopo hadi mwisho wa msimu huu, lakini watamchukua mshambuliaji wa Ajax na Uholanzi, Brian Brobbey (22), ikiwa watashindwa kufikia dili la kumsajili mshambulizi huyo wa Ureno. (***Florian Plettenberg***)

### NEIL ATAJWA SOKONI

WEST Ham inamfuatilia kiungo wa England, Dan Neil, lakini Sunderland inasita kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kuondoka katika msimu huu wa usajili wa wachezaji. (***Guardian***)


### VILLA YAMFUATA BADE

KLABU ya Aston Villa inataka kusajili mlinzi wa Ufaransa, Loic Bade mwenye umri wa miaka 24, kutoka Sevilla baada ya kumruhusu beki wa Brazil, Diego Carlos (31), kusajiliwa na Fenerbache. (***Express and Star***)

### BELAHYANE ANUKIA EPL

CHELSEA inamnyatia kiungo wa Hellas Verona na Morocco, Reda Belahyane, mwenye umri wa miaka 20, huku wakijiandaa kumuuza mchezaji wa Italia, Cesare Casadei (22). (***Gianluca di Marzio - kwa Kiitaliano***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RUBEN AANIKA SIRI HATIMA YA GARNACHO

**MANCHESTER,** England

### ●●● Kocha huyo asema lolote linaweza kutokea katika dirisha la...

RUBEN Amorim amekataa kuondoa uwezekano wa Alejandro Garnacho, kuondoka Manchester United kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili wa majira haya ya baridi.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 amekuwa akihusishwa na mpango wa kuihama United mwezi huu huku Napoli na Chelsea zikiwa na nia ya kumsajili.

**Alicheza vyema katika ushindi wa mabao 2-1 wa Ligi ya Europa dhidi ya Rangers hapo juzi.**

Lakini alipoulizwa kama unaweza kuwa mchezo wa mwisho wa raia hiyo wa Argentina kwenye Uwanja wa Old Trafford, Amorim hakupuuzia uvumi huo.

"Nimezingatia michezo na yuko hapa," alisema Amorim.

"Ni mchezaji wa Manchester United. Alikuwa muhimu sana kwetu leo (juzi) na tuone siku zijazo."

Vyanzo vimeiambia ESPN, United haimlazimishi Garnacho kuondoka klabuni hapo, lakini hali yao ya kifedha inamaanisha ofa ya kweli kwa mchezaji yeyote itazingatiwa.

Kupokea ada kwa Garnacho, mhitimu wa akademia, kutakuwa bonasi kwa United kwa sababu kunahesabiwa kama faida kamili kuhusiana na kufuata kanuni za faida na uendelevu za Ligi Kuu England.

"Nadhani anaimarika katika kila kipengele cha mchezo," aliongeza Amorim.

"Unaweza kuona hadi dakika 90 huwa yupo sawa, wakati mwingine anaonyesha kuchanganyikiwa na hiyo ni nzuri kwa sababu anataka zaidi.

"Nadhani ana uwezo wa kuwa bora zaidi katika kila hali ya mchezo. Ninachoweza kusema ni alielewa nilichokuwa najaribu kufanya, kilikuwa wazi kabisa, nataka tu kuwasaidia lakini mwishowe ni wao wanaofanya kazi hiyo."



# ARAÚJO AJIFUNGA BARCA HADI 2031

**BARCELOBA,** Hispania

RONALD Araújo ametia saini mkataba mpya na Barcelona na ataitumikia klabu hiyo ya Katalunya hadi nwaka, 2031 na kumaliza shaka yoyote juu ya mustakabali wake.

Mkataba wa awali wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ulipaswa kumalizika mwaka, 2026 na alikuwa anawaniwa na Juventus.

Lakini ESPN ilifichua hivi karibuni, mkutano na Mkurugenzi wa Michezo, Deco ulimshawishi abaki.

Araújo aliweka bayana kuhusu masharti yake mapya katika ofisi za klabu siku ya Alhamisi pamoja na Deco, Rais, Joan Laporta, na Makamu wa Rais, Rafa Yuste.

Beki huyo amerejea hivi karibuni kutokana na jeraha la misuli ya paja ambalo lilimfanya akae nje kwa kipindi cha kwanza cha msimu huu.

Na Pau Cubarsí na Iñigo Martínez ndio walikuwa na ushirikiano katikati ya safu ya nne ya nyuma ya Barca.

Jeraha la Martínez lilifungua mlango kwa Araujo kurejea kwenye kikosi, ingawa, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay ameanza mechi nne kati ya sita zilizopita za Barca.

Araújo alijiunga na Barca akitokea Boston River ya Uruguay mwaka 2018 na baada ya kudumu katika timu ya akiba ya klabu hiyo, amecheza zaidi ya mechi 150, akicheza jukumu muhimu waliposhinda taji la LaLiga msimu wa 2022-23.

## Juve yatangaza kumnasa Muani

**TURIN,** Italia

JUVENTUS imetangaza kukamilisha mkataba wa mkopo wa kumsajili mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Randal Kolo Muani, kwa muda uliosalia wa msimu wa 2024/25.

Huku Kylian Mbappe akiondoka PSG msimu uliopita wa joto, Muani amekuwa na wakati mgumu kwa dakika chache na hajashiriki kwa mabingwa hao wa Ligue 1 tangu Septemba mwaka jana.

Juventus wamelipa ada ya mkopo ya awali ya euro milioni moja, ambayo inaweza kupanda hadi euro milioni 2 zaidi kutegemeana na hali ya mchezaji mwenyewe.

Kolo Muani alianza kujulikana katika klabu ya Nantes, ikifuatiwa na kuhamia Eintracht Frankfurt kama mchezaji huru mnamo 2022.

Msimu wa mapumziko nchini Ujerumani, ambapo pia alikuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa kilichocheza Kombe la Dunia nchini Qatar.



Mchezaji huyo wa mwisho aliripotiwa kupewa ofa siku chache kabla ya Juve kukubaliana na PSG, huku kukiwa na nia ya ziada kutoka kwa Aston Villa, West Ham United na Everton.

# Pacha wa Salah asajiliwa Man City

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imekamilisha usajili wa mshambuliaji wa Eintracht Frankfurt, Omar Marmoush, klabu hiyo imetangaza.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri amehamia Uwanja wa Etihad kwa ada ya euro milioni 70 pamoja na nyongeza.

Vyanzo vimeambia ESPN kuwa malipo ya bonasi yaliyojumuishwa katika mpango huo yana jumla ya euro milioni 5.

Marmoush alisaini mkataba wa miaka minne na nusu Jumatano na anaweza kucheza mechi yake ya kwanza kwa City dhidi ya Chelsea leo Jumamosi.

Mkataba huo unafanya matumizi ya City katika dirisha la Januari kufikia euro milioni 145 pamoja na nyongeza.

"Hii ni siku ambayo sitaisahau," alisema Marmoush.

"Kusaini Manchester City, mojawapo ya timu bora zaidi duniani, ni hisia ya kushangaza. Nimefurahia, familia yangu inajivunia, na sote tuna furaha sana kuwa hapa Manchester.

"Pamoja na Pep, wafanyakazi wake na vifaa vya hali ya juu hapa, wachezaji wana kila kitu wanachohitaji ili kuwa bora. Hiyo ilinivutia sana nilipopata nafasi ya kuja hapa.




"Na siwezi kukataa pia nataka kushinda mataji na Man City imekuwa klabu yenye mafanikio zaidi nchini England kwa miaka mingi, kwa hivyo najua ninajiunga na mazingira ya ushindi na utamaduni wa kushinda.

"Nataka kujifunza kutoka kwa wafanyakazi na wachezaji wenzangu, na ninataka kuwa mwanachama wa thamani wa timu hii inayoshinda."

Marmoush anakuwa mchezaji wa tatu kusajiliwa na City katika dirisha la Januari baada ya kuwasili kwa Abdukodir Khusanov kutoka Lens na Vitor Reis kutoka Palmeiras.

Khusanov na Reis walianza mazoezi Jumanne na wanaweza pia kuwa kwenye kikosi dhidi ya Chelsea.

City pia ilimsajili fowadi Haaland kwa mkataba mpya wa miaka tisa na nusu wiki iliyopita.

Marmoush mwenye umri wa miaka 25, amewasili akiwa ameifungia Frankfurt mabao 20 msimu huu. Atavaa jezi namba 7 ya City.

"Omar ni mshambuliaji aliyekamilika na anayesisimua, na nina furaha kuungana nasi," alisema mkurugenzi wa soka wa City, Txiki Begiristain.

"Amekuwa na msimu bora, na kila mara tulipomtazama, amekuwa na ushawishi kwenye mechi.

"Ana sifa zote anazohitaji mshambulizi wa kiwango cha juu. Ana kasi na ufahamu wa hali ya juu, na ni wa kipekee mbele ya lango. Anaweza pia kucheza nafasi kadhaa tofauti."

## Simba sasa hesabu kubeba taji la CAF

INATOKA UK. 24

robo fainali, Kocha Fadlu (Davids) ataanza kutupa mazoezi yanayoendana na uzito wa michuano hiyo, pamoja na aina ya timu tunayokwenda kucheza nayo kama ambavyo amekuwa akifanya mara zote.

Mchezaji huyo alisema ndani ya kikosi hicho, mbali na kazi yake ya unahodha, moja ya kazi anayoifanya ni kuwafundisha wachezaji wapya utamaduni wa klabu yao na ,kiu' ya kufikia malengo.

"Wachezaji wote wapya wakifika kitu cha kwanza ni lazima ajue utamaduni wa timu, pili malengo ya klabu yakoje na hayo huwa tunapewa na viongozi kabla ya msimu kuanza, kila mchezaji anatakiwa alitambue hilo kila anapokuwa ndani na nje ya uwanja," alisema.

Mchezaji huyo aliyejiunga na Simba mwaka 2014 akitokea Kagera Sugar, amecheza robo fainali sita ndani ya misimu saba, Ligi ya Mabingwa mara nne kuanzia msimu wa 2018/19, 2020/21, 2022/23 na 2023/24, huku kati ya msimu wa 2021/22 na msimu huu, akicheza michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Simba, ambayo ilimaliza kinara wa Kundi A, inatarajia kucheza mechi ya robo fainali dhidi ya Stellenbosch ya Afrika Kusini , Asec Mimosas (Ivory Coast) au Al Masry ya Misri, ambazo zilimaliza kwenye nafasi ya pili kwenye makundi mengine.

Mechi za kwanza za hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika zitachezwa kati ya Machi 28 hadi 30, ambapo Simba ikitarajia kuanzia ugenini huku marudiano yakipangwa kufanyika kati ya Aprili 4 hadi 6, mwaka huu.



# DIDA, MAKAPU WASAJILIWA GEITA GOLD IKIOTA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa zamani wa Simba, Yanga, Azam FC, Deogratius Munishi ,Dida' na kiungo mkabaji, Said Makapu, wamejiunga na Geita Gold inayoshiriki Ligi ya Championship, imefahamika.

Geita Gold imewasajili wachezaji hao ili kuimarisha kikosi chao na hatimaye kufikia malengo ya kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Taarifa rasmi iliyotolewa na klabu hiyo jana imesema usajili wa nyota hao ulikamilika muda mfupi kabla ya dirisha la usajili kufungwa hapo Januari 15, mwaka huu, ambapo vilibaki vitu vichache tu vya kumalizia mchakato huo kabla ya kuwatangaza.

Klabu hiyo pia ilimtangaza Mohamed Muya, kuwa Kocha Mkuu wa kikosi hicho, akichukua nafasi ya Amani Josiah, ambaye kwa sasa amejiunga na Tanzania Prisons inayoshiriki Ligi Kuu Bara.

Muya ametua Geita Gold akitokea Fountain Gate, ambayo ilitangaza kumtimua muda mfupi baada ya kupokea kichapo kutoka kwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga.

„Tunawatambulisha kwenu Dida, kipa mzoefu nchini, pia tunamleta kwenu Makapu, kiungo bora na mkongwe ambaye ataongeza nguvu katika kikosi chetu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Mbali na kuzidakia timu hizo, Dida pia amezichezea Mtibwa Sugar, Lipuli, Namungo na akacheza soka la kulipwa nchini Afrika Kusini katika timu ya University of Pretoria.

Dida, ambaye amewahi kuitumikia Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), ametua Geita Gold kama mchezaji huru.

Makapu, ambaye amesajili kutoka Mashujaa FC, amewahi kuichezea Yanga, mwaka 2022, kabla ya kwenda Singida Big Stars.

Hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi ya Championship, Geita Gold, iliyoshuka daraja msimu uliopita, iko katika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 33 nyuma ya vinara Mbeya City yenye pointi 34 wakati vinara ni Mtibwa Sugar yenye pointi 38.



Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema (kushoto), akiongoza wachezaji wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa kuwakaribisha Alliance Girls katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), itakayochezwa Januari 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

## *Yanga: Copco FC mtatusamehe*

INATOKA UK. 24

ongezea uzoefu wachezaji wake.

"Msimu uliopita hautukufika hatua hii, tunaamini hadi hapa tulipo tumejifunza mengi, tunahitaji kupambana ili kuongeza jambo kwenye kikosi chetu, haitakuwa mechi rahisi kwa kila upande," aliongeza kocha huyo.

Katika mchezo wa leo, Yanga itatumia fursa kutaka kuwapoza na kuwafariji wanachama na mashabiki wao ambao wameumizwa na timu hiyo kushindwa kusonga mbele kwenye mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Ni mechi ya kiporo ambayo awali ilipaswa kufanyika Novemba, mwaka jana, lakini haikuchezwa kutokana na mabingwa hao watetezi kukabiliwa na michezo ya kimataifa.

Bingwa wa michuano hiyo hupata tiketi ya kuiwalilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# CECAFA yambeba Karia CAF

**Na Somoe Ng'itu**

WAJUMBE wa Mkutano Mkuu wa Baraza la Vyama vya Soka kwa Nchi za Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), wamempitisha Rais wa baraza hilo, Wallace Karia, kuwa mgombea pekee wa nafasi ya Ujumbe wa Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), imethibitishwa.

Uchaguzi Mkuu wa CAF unatarajiwa kufanyika Machi, mwaka huu nchini Morocco.

Karia, ambaye ni Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), alikuwa anatarajia kuchuana na Rais wa Shirikisho la Soka Uganda (FUFA), Moses Magogo.

„Magogo hatagombea nafasi ya ujumbe wa kamati ya utendaji ya CAF na sasa Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, Wallace Karia atakuwa mgombea pekee wa nafasi hiyo. Maana yake tayari Karia ameshapita katika nafasi hiyo," chanzo chetu kilisema.

Karia pia amethibitishwa kuwa mgombea pekee wa nafasi ya Urais katika uchaguzi ujao wa TFF, utakaofanyika baadaye mwaka huu.

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa TFF, waliazimia hivyo katika mkutano wa mwaka uliofanyika Desemba 21, mwaka jana mkoani Kilimanjaro.

CECAFA pia imetangaza kumuunga mkono Rais wa Shirikisho la Soka la Djibouti, Souleiman Waberi, kuwania nafasi ya ujumbe wa Kamati ya Utendaji wa FIFA, ambayo pia itafanya uchaguzi wake baadaye mwaka huu.

Waberi, mwamuzi wa zamani wa kimataifa, kwa sasa ni Makamu wa Tatu wa Rais wa CAF.

# Michezo

Jumamosi Januari 25, 2025

Nipashe





Ruben aanika siri hatima ya Garnacho

UKURASA 21

# YANGA: COPCO FC MTATUSAMEHE

## ●●● Ramovic aahidi kutumia nguvu, kasi ili kupata ushindi mnono...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

NGUVU, utulivu na kuweka dharau pembeni ndio kipaumbele cha mabingwa watetezi, Yanga kuelekea mechi ya raundi ya tatu ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Copco FC itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Yanga itashuka katika mchezo huo ikiwa na kumbukumbu ya kuondolewa kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kushindwa kupata ushindi walipowakaribisha MC Alger kutoka Algeria.

**Akizungumza kuhusu mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, alisema amejipanga kuingia uwanjani kucheza kwa nguvu na kasi kama walivyokuwa wakicheza kati ka michezo ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Ramovic alisema asitokee mtu au wapinzani wao wakadhani ataidharau mechi hiyo, badala yake ameelekeza nguvu 'kubwa' kwa kutumia silaha zote ili kushinda mchezo huo.

"Tunatakiwa kushinda mechi hii, pia kushinda kombe hili, Yanga siku zote ni timu ya ushindi, tunakutana na timu hii ndogo, hatutaidharau, hatuwezi kudharau timu yoyote ile, tutacheza kama tutavyocheza mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika na Ligi Kuu, kama tunavyocheza na timu yoyote kubwa, kwa nguvu kubwa, kwa kasi ya kutisha na kwa kutumia silaha zote tulizonazo ili kutinga hatua inayofuata," alisema Ramovic.

Naye Kocha Mkuu wa Copco yenye maskani yake jijini Mwanza, Lucas Mlingwa, alisema ataingia uwanjani akiwa na lengo la kutaka kutonesha kidonda ambacho kiliachwa na 'Waarabu.'




Kiungo mshambuliaji wa kimataifa wa Yanga, Stephane Aziz Ki (kulia), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya raundi ya tatu ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Copco FC itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

Mlingwa alikiri Yanga ni timu kubwa na bora, lakini wataingia na mkakati maalum, ambao utafanya kazi waliokusudia ili kupata matokeo chanya.

"Tumejiandaa vya kutosha kwa ajili ya hii mechi, wachezaji wameniambia wako tayari kwa ajili ya kupambana na tunakwenda kucheza tukiwa na malengo ambayo tumejiwekea ili kuyatimiza kesho (leo).

Tunaamini Yanga ni timu bora, hilo kila mtu analijua na hiyo ni faida kubwa kwetu kucheza na mpinzani unayejua uwezo wa kiwango chake, huwezi kuingia kwenye Uwanja wa KMC Complex, kucheza nao mshindane, uwezo wa mchezaji mmoja mmoja, wana kiwango bora kuliko sisi, kwa maana hiyo tumekuja na mpango mkakati, yaani kufidia kile ambacho hatuna, kupunguza eneo lao la kucheza, sisi tuwe na namba kubwa ya watu katika kila eneo, ina maana wachezaji wetu ni lazima wakimbie sana," alisema kocha huyo.

Aliongeza wanahitaji kuendelea kupata matokeo mazuri msimu huu ili kuwa-

INAENDELEA UK. 23

## Simba sasa hesabu kubeba taji la CAF

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', amefichua malengo ya timu na wachezaji wa timu hiyo waliojiwekea msimu huu ni kufika hatua ya fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika au kulitwaa kombe la michuano hiyo.

Vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara ndio wawakilishi pekee wa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayosimamiwa na kuandaliwa na CAF.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Zimbwe Jr, beki wa kushoto wa timu hiyo, alisema malengo hayo hayakuwa kutinga robo fainali, bali ni kufika mbali ikiwamo ndoto za kubeba ubingwa.

Nyota huyo alisema kutinga hatua ya robo fainali kwao ni njia ya kupita kuelekea kwenye mafanikio wanayoyahitaji msimu huu.

Alisema yeye binafsi ameweka rekodi ya kufika robo fainali mara sita katika michuano ya kimataifa, hivyo hawezi tena kushtuka akifika hapo, badala yake anataka kusonga mbele zaidi msimu huu.

"Ni jambo kubwa sana kwangu kutimiza robo fainali sita za kimataifa zinazotambuliwa na CAF, kwa sababu wapo ambao wanatamani kuwa hapa, lakini hawafikii malengo.

Niseme tu safari hii siyo tena robo fainali, ni fainali, kuna matarajio yangu binafsi ambayo nataka nivuke hatua ambayo siku zote naishia, malengo ya klabu tuliopewa na viongozi wetu pamoja na yetu sisi wachezaji wote ni kuhakikisha tunafika fainali na ikiwezekana kutwaa taji lenyewe," alisema Zimbwe Jr.

Aliongeza kwa sasa wanafanya mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Kombe la FA na Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini akiwa na uhakika muda utakapofika wataanza kujiandaa kikamilifu na michezo miwili hatua ya robo fainali.

"Nadhani tukikaribia kucheza

INAENDELEA UKURASA 23


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042